BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2017

# MAARIFA YA JAMII

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI 2017

# MAARIFA YA JAMII

Kimechapwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2017

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................... iv
1.0 UTANGULIZI ........................................................................ 1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI ........................................................................ 3
2.1. Sehem A: Uraia ................................................................. 3
2.2. Sehemu B: Historia.......................................................... 26
2:3 Sehemu C: Jiografia .......................................................... 56
3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA ......................................................................... 78
4.0 HITIMISHO .......................................................................... 81
5.0 MAPENDEKEZO .................................................................. 82
KIAMBATISHO ......................................................................... 83

## DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi 2017 kwa somo la Maarifa ya Jamii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu. Majibu ya watahiniwa katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha maarifa, stadi na mielekeo ambayo watahiniwa waliweza kupata au kutopata katika kipindi cha miaka saba ya Elimu ya Msingi.

Katika taarifa hii, mambo mbalimbali ambayo yamechangia watahiniwa kushindwa kujibu maswali kwa usahihi yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa yafuatayo yamechangia wanafunzi kushindwa kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi: Kushindwa kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali, kutokuwa na ufahamu kabisa wa baadhi ya mada, kushindwa kuhawilisha mafunzo na kutojibu baadhi ya maswali au kutofuata maelekezo ya mtihani. Uchambuzi wa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali walizoonesha watahiniwa wakati wa kujibu maswali zimeainishwa. Aidha, ulinganifu wa kufaulu kati ya mwaka 2016 na 2017 kwa kila mada umefanyika ili kuonesha kupanda au kushuka kwa kufaulu katika kila mada.

Baraza la Mitihani Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa dosari zilizoainishwa katika taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi ili kuongeza ujuzi na maarifa kwa wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi.

Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Baraza la Mitihani litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa jumla ambayo yatasaidia kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa siku zijazo.



**Dkt. Charles E. Msonde**

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE 2017) ulifanyika kati ya tarehe 06 na tarehe 07 ya mwezi Septemba, 2017. Katika mtihani huo, somo la Maarifa ya Jamii lilifanyika tarehe 06/09/2017. Jumla ya watahiniwa **916,885** walisajiliwa kufanya mtihani huu ambapo watahiniwa **909,902** sawa na asilimia **99.2** walifanya mtihani huo katika somo la Maarifa ya Jamii. Uchambuzi wa majibu ya mtihani wa Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa watahiniwa **570,781** sawa na asilimia **62.73** walifaulu mtihani huo katika somo hilo.

Somo la Maarifa ya Jamii katika mtihani wa PSLE, 2017 lilikuwa na jumla ya maswali 50 ya kuchagua yaliyokuwa yamegawanyika katika sehemu kuu tatu: sehemu A: Uraia – iliyokuwa na maswali 14, sehemu B: Historia – iliyokuwa na maswali 18 na sehemu C: Jiografia iliyokuwa na maswali 18. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika sehemu zote tatu. Aidha, mtahiniwa alipewa machaguo matano katika kila swali, ambayo kati yake kulikuwa na jibu sahihi. Mtahiniwa alitakiwa kuchagua jibu sahihi na kisha kuweka kivuli katika herufi ya jibu sahihi katika fomu ya kujibia (OMR).

Katika uchambuzi huu, idadi ya watahiniwa na asilimia yao katika kila chaguo itaoneshwa. Ubora wa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika kila swali utategemea idadi ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi. Katika uchambuzi huu pia, sababu za watahiniwa kuchagua jibu, vipotoshi, kutojibu baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja zitabainishwa.

Katika uchambuzi huu, ukokotoaji wa kiwango cha ufaulu utategemea idadi ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi kama ifuatavyo: endapo watahiniwa asilimia 0 hadi 39 ndio watakaokuwa wamechagua jibu sahihi, ufaulu katika swali au mada hiyo utaelezwa kuwa ni hafifu. Kwa upande mwingine, endapo watahiniwa kati ya asilimia 40 hadi 59 watakuwa wamechagua jibu sahihi, ufaulu katika swali hilo utaelezwa kuwa ni wa wastani. Aidha, ufaulu katika swali au mada utaelezwa kuwa mzuri endapo watahiniwa asilimia 60 au zaidi watakuwa wamechagua jibu sahihi.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI

### 2.1. Sehem A: Uraia

**Swali la 1:** Mwakilishi wa wananchi katika vikao vya Halmashauri za Jiji, Manispaa na Miji ni

A Afisa Mtendaji kata.

B Mwenyekiti wa kijiji.

C Diwani.

D Mratibu wa Elimu kata.

E Katibu Kata.

**Jedwali Na. 1: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| CHAGUO | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | **117936** | **134485** | **584872** | **40818** | **28905** | **10068** |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | **12.86** | **14.66** | **63.78** | **4.45** | **3.15** | **1.10** |

Swali hili lilitoka katika mada ya Serikali za Mitaa. Swali lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu mwakilishi wa wananchi katika vikao vya Halmashauri ya Jiji, Manispaa na Miji.

Swali hili lilijibiwa vizuri kama inavyoonekana katika jedwali Na. 1 ambapo jumla ya watahiniwa 584,872 (63.78%) walichagua jibu sahihi *C, Diwani*. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na uelewa kuhusu kazi na majukumu ya madiwani na viongozi wengine katika Halmashauri za Jiji, Manispaa na Miji. Aidha, kipotoshi *A, Afisa Mtendaji Kata* kiliwavutia watahiniwa 117,936 (12.8%). Watahiniwa

hao pengine walikosea kwa sababu Afisa Mtendaji Kata ni mtu wanayemuona akifanya shughuli kila siku katika maeneo yao, hivyo wakafikiri ndiye mwakilishi wa wananchi katika vikao vya halmashauri tajwa katika swali. Aidha, watahiniwa wengine 134,485 (14.66%) walivutiwa na kipotoshi *B, Mwenyekiti wa Kijiji*. Watahiniwa hao huenda walichagua kipotoshi hicho wakifikiri ni jibu sahihi kutokana na Mwenyekiti wa kijiji kuwa kiongozi aliye karibu zaidi na wananchi katika ngazi za chini za utawala katika serikali za mitaa. Pia watahiniwa wengine 28,905 (3.15%) walichagua *E, Katibu kata*. Hili halikuwa jibu sahihi kwa kuwa katika muundo wa sasa wa serikali za mitaa hakuna cheo cha Katibu kata. Kwa hiyo Watahiniwa hao walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu muundo wa serikali za mtaa. Watahiniwa wengine 40,818 (4.45%) walichagua *D, Mratibu Elimu kata* kutokana na kumwona Mratibu Elimu Kata akitembelea shule zao mara kwa mara.

Kuwepo kwa watahiniwa wengi waliotaja chaguo sahihi kunaashiria kuwa mada kuhusu Serikali za Mitaa na muundo wake ilieleweka vizuri kwa watahiniwa wengi, na hasa kuhusu mwakilishi wa wananchi katika vikao vya Halmashauri za Jiji, Manispaa na Miji hapa Tanzania.

**Swali la 2**: Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni ni


A Spika wa Bunge
B Waziri wa Katiba na sheria
C Rais
D Waziri Mkuu
E Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Serikali Kuu.* Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kubaini kiongozi wa shughuli za serikali Bungeni.

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 438,938 (47.86%) waliweza kuchagua jibu sahihi *D, Waziri Mkuu.* Hii inaashiria kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa sahihi kwa mada husika, hasa majukumu ya Waziri Mkuu awapo Bungeni.

Watahiniwa wengine 307,749 (33.6%) walivutiwa na kipotoshi *A Spika wa Bunge*. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa kazi ya Spika ni kuongoza Bunge na si serikali. Uchaguzi wa kipotoshi hiki unaashiria kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa mzuri wa mihimili ya dola na viongozi wake. Hata hivyo, watahiniwa 37,437 (4.1%) walichagua *B, Waziri wa Katiba na Sheria*. Pengine watahiniwa hao walidhani waziri wa Katiba na Sheria ndiye kiongozi wa shughuli za serikali Bungeni kutokana na jinsi anavyofafanua mambo mbalimbali ya kikatiba na kisheria ndani ya Bunge. Watahiniwa 87,128 (9.5%) walichagua *C, Rais* na wengine 35,721 (3.9%) walichagua *E, Mwanasheria Mkuu wa Serikali*. Watahiniwa hao pengine walifikiri kuwa, kwa vile maafisa hao wana nyadhifa za juu serikalini, pia ni viongozi wa shughuli za serikali Bungeni.

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha chini ya asilimia 50 hali iliyoashiria kuwa watahiniwa wengi hawakuielewa mada vizuri na ndio maana walivutiwa na vipotoshi mbalimbali.




**Kielelezo Na. 1**: *Kiwango cha kufaulu katika swali hili ni cha wastani kwani asilimia 47.86 ya watahiniwa waliweza kuchagua herufi ya jibu sahihi.*

**Swali la 3:** Nani ni kiongozi Mkuu wa shughuli za kila siku za Halmashauri ya Manispaa?

A Mwenyekiti wa Halmashauri ya Manispaa

B Diwani

C Meya

D Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya

E Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa

**Jedwali Na. 2: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| CHAGUO | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 186,860 | 137,563 | 288,876 | 97667 | 193194 | 12924 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 20.38 | 15.00 | 31.50 | 10.65 | 21.07 | 1.40 |

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye mada ya *Serikali za Mitaa*. Watahiniwa walitakiwa kubaini kiongozi mkuu wa shughuli za kila siku za Halmashauri ya Manispaa.

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu ambapo idadi ya watahiniwa 710, 966 (77.53%) walishindwa kubaini jibu sahihi. Kati ya watahiniwa hao 186,860 (20.4%) walichagua kipotoshi *A, Mwenyekiti wa Halmshauri ya Manispaa*. Hili haliwezi kuwa jibu sahihi kwa sababu kazi ya Mwenyekiti ni kuitisha na kuongoza vikao vya Halmashauri ya Manispaa na si vinginevyo. Hata hivyo, watahiniwa wengine 137,563 (15%) walichagua *B, Diwani.* Watahiniwa hao walishindwa kujua kuwa Diwani ni mwakilishi wa wananchi katika vikao vya Halmashauri za Manispaa, Miji, Jiji na Wilaya na si vinginevyo. Watahiniwa 288,876 (31.5%) waliochagua herufi *C, Meya* walishindwa kuelewa kuwa Meya ni Kiongozi Mkuu wa Manispaa na Majiji na wala si mtendaji wa shughuli za kila siku za manispaa. Watahiniwa 97,667 (10.6%) waliochagua *D, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya* hawakubaini kuwa cheo hicho kwa sasa hakipo kwenye mfumo wa watendaji wa Manispaa.

Idadi ndogo ya watahiniwa 193,194 (21.07%) waliweza kubaini jibu sahihi *E, Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa*. Watahiniwa hao walidhihirisha uelewa wao kuhusu shughuli za watendaji wa manispaa na ndio maana hawakusumbuliwa na vipotoshi vilivyokuwepo.


Kuwepo kwa idadi kubwa ya watahiniwa 710,966 (77.53%) walioshindwa swali hili kunaashiria kuwa walikosa uelewa wa

kutosha kuhusu mada husika, hasa muundo wa utawala katika Manispaa na majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa.

**Swali la 4:** Ni muhimu kuzingatia jambo moja kati ya yafuatayo wakati wa kuimba Wimbo wa Taifa:

A kushika bendera ya Taifa
B kusimama na kutulia
C kuangalia upande wa kulia
D kuinua juu mkono wa kulia
E kukaa chini kwa utulivu

Swali hli lilitoka katika mada ya *Alama za Taifa.* Liliwataka watahiniwa kubainisha kutoka katika machaguo matano waliyopewa jambo linalopaswa kuzingatiwa wakati wa kuimba Wimbo wa Taifa. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa umeoneshwa katika Kielelezo Na. 2 hapo chini.




**Kielelezo Na. 2** *Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani 85.24% ya watahininiwa waliweza kuchagua jibu sahihi.*

*Kielelezo Na. 2* hapo juu kinaonesha kuwa, asilimia 85.2 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi swali hili kwa kuchagua jibu sahihi ambalo ni *B, kusimama na kutulia*. Hii inadhihirisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa Wimbo wa Taifa ni alama ya taifa inayoonesha utambulisho wa Taifa la Tanzania, hivyo unahitajika kuimbwa kwa heshima na utulivu. Watahiniwa waliweza kujibu swali hili kwani ni mada iliyofundishwa kwa nadharia na vitendo wanapokuwa shuleni hasa mikusanyiko ya asubuhi (*morning assembly)* na wanapokuwa katika matukio muhimu shuleni.

Hata hivyo, asilimia 5.2 ya watahiniwa walichagua *A, kushika bendera ya Taifa* ambalo halikuwa jibu sahihi, kwani bendera hupandishwa katika mlingoti. Watahiniwa wengine (2.2%) walichagua kipotoshi *C, kuangalia upande wa kulia* kwani kwa kawaida watu husimama na kuangalia mbele. Watahiniwa wachache (4.3%) walikosa kwa kuchagua *D, kuinua juu mkono wa kulia,* ambapo tukio hilo halifanyiki wakati wa kuimba wimbo wa taifa bali hutumika wakati wa kuapishwa kwa viongozi wa serikali na watumishi mbali mbali. Watahiniwa wachache (2.0%) walikosa maarifa kabisa kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa kuimba wimbo wa taifa na hivyo kuchagua *E, kukaa chini kwa utulivu* ambalo halikuwa jibu sahihi*.*

**Swali la 5:** Alama inayowakilisha wafanyakazi katika Nembo ya Taifa ni

A jembe
B mkuki
C pembe za ndovu
D mwenge wa uhuru
E shoka

**Jedwali Na. 3: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| CHAGUO | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 519,107 | 49,479 | 74,140 | 125,340 | 136,388 | 12,630 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 56.60 | 5.40 | 8.08 | 13.67 | 14.87 | 1.40 |

Swali hili lililenga kupima ufahamu wa watahiniwa kuhusu tafsiri ya alama mbalimbali zilizopo kwenye nembo ya Taifa. Nembo ya Taifa ni beji maalum ya serikali inayotumika katika ofisi za serikali, kwenye nyaraka, fedha na kwenye bendera ya Rais. Aidha, nembo ya Taifa inayowakilisha wafanyakazi ni shoka.

Kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 3, watahiniwa 768,066 (83.75%) walishindwa kuchagua jibu sahihi. Kati ya watahiniwa hao, 56.6% walichagua *A, jembe* alama inayowakilisha wakulima. Asilimia 8.1 walichagua *C, pembe za ndovu* ambazo zinaonesha mali asili za nchi; asilimia 13.7 walichagua *D, mwenge wa uhuru* ambao unawakilisha uhuru wa nchi na asilimia 5.4 walichagua *B, mkuki* ambao huwakilisha ulinzi na utawala na uhuru wa Tanzania.

Ni asilimia 14.9 tu ya watahiniwa ndio walioweza kuchagua jibu sahihi *E, shoka* kama alama mbayo huwakilisha wafanyakazi kwani shoka ni kifaa kinachotumiwa na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza uchumi wa nchi. Hii inaashiria kuwa watahiniwa wengi hawakuwa na ufahamu sahihi wa tafsiri ya alama zinazoonekana kwenye Nembo ya Taifa.

**Swali la 6:** Waendao kwa miguu wanashauriwa kutembea barabarani kwa


A kutumia upande wa kulia wa barabara.
B kutumia upande wa kushoto wa barabara.
C kuangalia upande wa kulia na kushoto wa barabara.
D kushikana mikono.
E kuangalia taa za usalama wa barabarani tu.

Swali hili lilitokana na mada ya *Ulinzi na Usalama.* Katika swali hili, watahiniwa walitakiwa kubainisha upande sahihi ambao watembea kwa miguu wanatakiwa kutumia wakati wakiwa barabarani.

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa 683,608 (74.53%) walishindwa kuchagua jibu sahihi. Kati ya hao, watahiniwa 343,995 (37.5%) walichagua *C, kuangalia upande wa kulia na kushoto wa barabara* ambayo ni stadi inayotumika wakati wa kuvuka barabara na sio wakati wa kutembea barabarani. Kipotoshi *B, kutumia upande wa kushoto wa barabara* kiliwavutia watahiniwa 193,131 (21.1%) ambao pengine walifikiri watembea kwa miguu hutembea upande wa kushoto kama wanaoendesha vyombo vya moto. Aidha, watahiniwa 115,353 (12.6%) walichagua kipotoshi *E, kuangalia taa za usalama wa barabarani tu* kwani kiuhalisia taa za usalama barabarani hutumika zaidi kwenye makutano ya baadhi ya barabara za mjini na hivyo siyo wakati wote na mahali pote zinaweza kutumika kwani taa hizo haziko kila mahali. Watahiniwa 31,129 (3.4%) walichagua *D, kushikana mikono* ambayo ni stadi inayotumika pale tunapowavusha barabara watoto, walemavu na wazee.

Watahiniwa wengi kushindwa kuchagua jibu sahihi kunaashiria ufinyu wa maarifa waliyokuwa nayo, hasa katika kipengele cha usalama barabarani.

Watahiniwa 221,647 (24.17%) waliweza kuchagua jibu sahihi *A, kutumia upande wa kulia wa barabara*. Hii inadhihirisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mzuri wa elimu ya usalama barabarani na matumizi sahihi ya barabara. Kwa ujumla, watahiniwa wengi walikosa swali hili kwa sababu ya uelewa mdogo na uzoefu usio sahihi wa matumizi ya barabara.




**Kielelezo Na. 3**: *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kwani ni asilimia 24.17 tu ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi.*

**Swali la 7**: Faida za ulinzi na usalama shuleni ni pamoja na

A kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa.

B kuweka mazingira ya ujifunzaji katika hali ya amani na utulivu.

C kuhakikisha walimu na wanafunzi wanafika shuleni kwa wakati.

D kupanua wigo wa demokrasia shuleni.

E kusaidia ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu.

**Jedwali la 4: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| CHAGUO | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 48,684 | 649,281 | 84,644 | 76,114 | 47,441 | 10,920 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 5.31 | 70.80 | 9.23 | 8.30 | 5.17 | 1.20 |

Swali hili lilitoka katika *Mada ya Ulinzi na Usalama* na lilipima uelewa wa mtahiniwa katika kutambua faida za ulinzi na usalama shuleni. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 649,281 (70.80%) walichagua *B, kuweka mazingira ya ujifunzaji katika hali ya amani na utulivu* ambalo lilikuwa jibu sahihi. Watahiniwa waliweza kubaini jibu sahihi kwa kuhusisha swali na mazingira halisi shuleni ambako bila ulinzi na usalama utulivu na amani vitatoweka na ujifunzaji hauwezi kufanyika.

Watahiniwa wengine 48,648 (5.3%) walichagua kipotoshi *A, kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa* jibu ambalo halihusiki na ulinzi na usalama shuleni. Watahiniwa wengine 84,644 (9.2%) walichagua kipotoshi *C, kuhakikisha walimu na wanafunzi wanafika shuleni kwa wakati*. Hao walikosea kwa kuwa kazi ya muda

wa walimu na wanafunzi kufika kazini huwekwa na utawala wa shule na hauhusiani na ulinzi na usalama shuleni. Hata hivyo, watahiniwa 76,114 (8.3%) walivutiwa na kipotoshi *D, kupanua wigo wa demokrasia shuleni* ingawaje walishindwa kutambua kuwa demokrasia shuleni hupanuliwa kwa kuhusisha wanafunzi kwenye ufanyaji wa maamuzi katika masuala mbali mbali. Masuala hayo ni kama vile uchaguzi wa viongozi wao, kazi ambayo haihusiani na madhumuni ya ulinzi na usalama shuleni. Mwisho, watahiniwa wengine 47,441 (5.2%) walichagua kipotoshi *E, kusaidia ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu* ambalo kimsingi ni jukumu la serikali za mitaa husika katika maeneo yao na halihusiani na madhumuni ya ulinzi na usalama shuleni.

Kwa kuhitimisha watahiniwa wengi walifaulu katika swali hili kwa kuwa walikuwa na maarifa na uelewa wa kutosha wa mada husika yaani ulinzi na usalama na mchango wake shuleni.

**Swali la 8:** Utawala bora unaweza kuimarishwa shuleni kwa njia zifuatazo isipokuwa

A wanafunzi kuchagua viongozi wao.

B wanafunzi kufahamu mapato na matumizi ya shule.

C viongozi wa wanafunzi kuwa na maamuzi ya mwisho katika jambo lolote.

D viongozi wa wanafunzi kuheshimu mawazo ya wanafunzi wenzao.

E wanafunzi kupokea ushauri kutoka kwa walimu wao.

**Jedwali Na 5: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| CHAGUO | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 74,768 | 208,190 | 502,608 | 50,539 | 69,280 | 11,699 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 8.15 | 22.70 | 54.81 | 5.51 | 7.55 | 1.30 |

Swali hili lilitokana na mada ya *Misingi ya Demokrasia*. Swali lilipima uelewa wa watahiniwa katika kutambua njia ambazo haziwezi kutumika kuimarisha utawala bora shuleni. Watahiniwa walifaulu katika swali hili kwa kiwango cha wastani ambapo watahiniwa 502,608 (54.81%) walichagua chaguo sahihi *C, viongozi wa wanafunzi kuwa na maamuzi ya mwisho katika jambo lolote*. Watahinwa hao waliweza kutafsiri swali vizuri na walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya njia zinazoimarisha na zisizoimarisha utawala bora shuleni. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa siyo katika mambo yote viongozi wa wanafunzi wanapaswa kuwa waamuzi wa mwisho.

Watahiniwa waliokosa swali hili walikosa kwa kuchagua machaguo yafuatayo: watahiniwa 74,768 (8.2%) walichagua *A, wanafunzi kuchagua viongozi wao* ambayo kimsingi huboresha utawala bora shuleni na si kinyume chake. Pengine walifanya hivyo kwa kukosa umakini katika kutambua matakwa ya swali. Hata hivyo watahiniwa wengine 208,190 (22.7%) walivutiwa na kipotoshi *B, wanafunzi kufahamu mapato na matumizi ya shule*. Suala hili kimsingi huboresha utawala bora shuleni na si vinginevyo kama walivyojibu watahiniwa. Watahiniwa wengine 50,539 (5.5%) walichagua *D, viongozi wa wanafunzi kuheshimu mawazo ya wanafunzi wenzao*. Kiukweli, hii ni dhana sahihi ya utawala bora shuleni na si vinginevyo

kama walivyofikiria. Mwisho, watahiniwa 69,260 (7.6%) walichagua *E, wanafunzi kupokea ushauri kutoka kwa walimu wao* jambo ambalo ni muhimu katika kuimarisha utawala bora shuleni. Uchaguzi wa vipotoshi hivi pengine ulitokana na watahiniwa hao kukosa maarifa kuhusu misingi ya demokrasia katika ngazi ya shule.

Kwa ujumla swali hili lilijibiwa vizuri kutokana na watahinwa wengi kuweza kubaini matakwa ya swali na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu misingi ya demokrasia.

**Swali la 9**: Lipi kati ya makundi yafuatayo linawakilisha vyama vya siasa vilivyosajiliwa Tanzania?


A CCM, CHADEMA na TAMWA
B CCM, CHADEMA na LHCR
C CHADEMA, CCM na NCCR
D CHADEMA, MEWATA na TAMWA
E MEWATA, CCM na TAMWA

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Demokrasia* na liliwataka watahiniwa kubainisha kundi la vyama vya siasa vilivyosajiliwa nchini Tanzania.

Kwa ujumla, swali hili lilijibiwa katika kiwango cha wastani ambapo watahiniwa 519,465 (56.64%) waliweza kubaini jibu sahihi *C, CHADEMA, CCM na NCCR*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa sahihi kuhusu majina ya vyama vya siasa vilivyosajiliwa Tanzania.

Hata hivyo, watahiniwa waliobakia 385,925 (42.08%) walichagua vipotoshi kama ifuatavyo: watahiniwa 239,614 (26.13%) walichagua *A, CCM, CHADEMA na TAMWA* bila kujua kuwa TAMWA ni chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania, na hivyo sio chama cha Siasa. Wengine 67,029 (7.31%) walichagua *B, CCM, CHADEMA na LHRC* bila kujua kuwa LHRC ni kituo cha Haki za Binadamu na si chama cha siasa.  Aidha, wengine 33,501 (3.65%) walichagua *D, CHADEMA, MEWATA na TAMWA* bila kujua kuwa MEWATA ni chama cha Madaktari Wanawake Tanzania na TAMWA ni Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania, hivyo hivi sio vyama vya siasa. Mwisho, watahiniwa 45,780 (4.99%) walichagua *E, MEWATA, CCM na TAMWA* pasipo kujua kuwa MEWATA na TAMWA sio vyama vya siasa bali ni baadhi ya vyama vya Wanawake Tanzania.

Kwa ujumla, swali hili lilijibiwa vizuri kutokana na watahiniwa wengi kuwa na umakini na uelewa wa kutosha kuhusu vyama vya siasa vilivyosajiliwa nchini Tanzania. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa waliochagua vipotoshi vingine walionesha kutokuwa na uelewa mzuri wa dhana ya vyama vya siasa, hivyo kushindwa kutofautisha kati ya vyama vya siasa na vyama visivyo vya siasa katika machaguo yaliyotolewa.




**Kielelezo Na. 4**: *Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kilikuwa cha wastani kwani asilmia ya watahiniwa walioweza kuchagua jibu sahihi ni asilimia 56.64.*

**Swali la 10**: Lengo kuu la kuanzishwa mfumo wa vyama vingi vya siasa hapa Tanzania ni

A kuwavutia wawekezaji kutoka nje ya nchi.

B kupanua na kuimarisha demokrasia.

C kuongeza idadi ya vyama vya siasa.

D kutekeleza masharti ya wawekezaji wa kimataifa.

E kuunda serikali ya umoja wa kitaifa.

**Jedwali Na. 6: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| CHAGUO | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 46,505 | 589,698 | 89,258 | 48,281 | 131,380 | 11,962 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 5.07 | 64.30 | 9.73 | 5.26 | 14.33 | 1.30 |

Swali hili lilitungwa kutoka mada ya *Demokrasia* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu lengo kuu la kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa hapa Tanzania.

Swali lilijibiwa vizuri ambapo watahiniwa 589,698 (64.30%) walichagua jibu sahihi *B, kupanua na kuimarisha demokrasia*. Watahiniwa hao waliweza kubaini jibu sahihi kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sababu za kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini Tanzania.

Hata hivyo, watahiniwa wengine walitoa majibu yasiyo sahihi kama ifuatavyo: 46,505 (5.07%) walichagua *A, kuwavutia wawekezaji kutoka nje ya nchi*. Pengine walifikiri mfumo wa vyama vingi vya siasa ni utaratibu rasmi uliolenga kupanua uchumi kwa kuwakaribisha wawekezaji toka nje. Aidha, watahiniwa 89,258 (9.73%) walichagua *C, kuongeza idadi ya vyama vya siasa*. Huenda watahiniwa hao walisahau kuwa kilichohitajika kama jibu sahihi ni lengo la kuanzishwa kwa vyama vingi na wala sio maana ya vyama vingi kama walivyoandika. Hata hivyo, watahiniwa 48,281 (5.26%) walichagua *D, kutekeleza masharti ya wawekezaji wa kimataifa*. Pengine watahiniwa hao walifikiri kuwa mfumo wa vyama vingi ni utaratibu rasmi ulioanzishwa ili kusikiliza na kutekeleza masharti ya wawekezaji wa kimataifa hapa nchini badala ya kupanua demokrasia nchini. Mwisho, watahiniwa 131,380 (14.33) waliochagua *E, kuunda serikali ya umoja wa kitaifa*. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa umoja wa kitaifa umekuwepo Tanzania tangu tupate uhuru na haukutokana na kuanzishwa kwa vyama vingi Tanzania.

Kuwepo na watahiniwa wengi waliofaulu swali hiili ni kielelezo kuwa palikuwa na ufundishwaji na uelewa sahihi wa mada ya *Demokrasia*.

**Swali la 11**: Ni mila zipi zinaweza kueneza UKIMWI?

A Ngoma za utamaduni
B Miiko ya vyakula
C Kuzaa watoto wengi
D Kurithi wajane
E Mahari


Swali hili lilitungwa kutoka kwenye mada ya *Utamaduni Wetu* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu mila zinazoweza kueneza UKIMWI.

Swali hili lilijibiwa vizuri na watahiniwa 638,526 (69.63%) waliochagua jibu sahihi *D, kurithi wajane* chaguo linalodhihirisha kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya UKIMWI na jinsi ugonjwa huu unavyoweza kuenezwa kwa mila potofu.

Watahiniwa waliokosa swali hili walitoa majibu yasiyo sahihi kama ifuatavyo: 75,588 (8.24%) walichagua *A, ngoma za utamaduni*. Pengine walifikiria hivyo kutokana na kuwa baadhi ya ngoma za utamaduni huchochea matendo ya zinaa ambayo hueneza UKIMWI. Watahiniwa wengine 58,941 (6.43%) walichagua *B, miiko ya vyakula*. Watahiniwa hao walidhani kila mila potofu hueneza UKIMWI jambo ambalo sio sahihi. Watahiniwa 85,141 (9.28%) walichagua *C, kuzaa watoto wengi.* Pengine watahiniwa hao walihusisha dhana ya kuzaa watoto wengi kama mila inayoweza kueneza UKIMWI. Watahiniwa wengine 46,707 (5.09%) walichagua

*E, mahari* ambayo ni mali anayotoa mwanaume kuwapa wazazi wa mwanamke anayetarajia kumuoa na siyo mila ambayo hueneza UKIMWI.

Watahiniwa wengi waliweza kuonesha uelewa mzuri wa jinsi UKIMWI unavyoweza kuenezwa na mila potofu. Hii inaashiria kuwa watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa mada husika kwa kadiri ya mahitaji ya swali kama inavyojidhihirisha katika kielelezo Na. 5.




**Kielelezo Na. 5***: Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani asilimia 69.63 ya watahiniwa waliweza kubaini jibu sahihi.*

**Swali la 12:** Kuna makundi mangapi ya uoto wa asili?

A Matatu B Manne C Mawili

D Matano E Sita

**Jedwali Na. 7: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| CHAGUO | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 138,414 | 85,301 | 585,358 | 57,395 | 38,712 | 11,904 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 15.09 | 9.30 | 63.83 | 6.26 | 4.22 | 1.30 |

Swali hili ni miongoni mwa maswali ambayo hayakujibiwa vizuri na watahiniwa, kwani jumla ya watahiniwa 766,766 (83.61%) walishindwa kubaini jibu sahihi. Hivyo, walichagua machaguo yasiyo sahihi ambapo asilimia 9.3 walichagua kipotoshi *B, Manne,* asilimia 63.8 walichagua *C, Mawili,* asilimia 6.3 walichagua *D, Matano* na asilimia 4.2 walichagua *E, Sita.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivi walikosa maarifa ya kutosha kuhusu makundi ya uoto wa asili.

Ni asilimia 15.1 tu ya watahiniwa waliweza kuchagua herufi ya jibu sahihi *A, Matatu.* Kuwepo kwa asilimia ndogo ya watahiniwa walioweza kubaini jibu sahihi kunaonesha kuwa kuna tatizo la la ufundishaji na ujifunzaji wa mada ndogo ya *Rasilimali Kuu za Taifa* ambayo ni sehemu ya mada kuu ya *Uchumi Wetu.*

**Swali la 13**: Lengo kuu la mabadiliko ya Katiba ya mwaka 1962 nchini Tanzania yalikuwa

A kuunda serikali ya umoja wa kitaifa.
B kuunda serikali ya shirikisho.
C kuunda serikali ya mitaa.
D kuunda serikali ya Jamhuri.
E kuunda serikali ya mpito.

**Jedwali Na. 8: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| CHAGUO | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 255,561 | 63,159 | 113,710 | 398,703 | 72,360 | 13,591 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 27.87 | 6.89 | 12.40 | 43.48 | 7.89 | 1.50 |

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Swali lilipima uelewa wa mtahiniwa kuhusu lengo kuu la mabadiliko ya Katiba ya mwaka 1962 nchini Tanzania.

Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani (Tazama Jedwali Na. 8 hapo juu) ambapo watahiniwa 398,703 (43.48%) walichagua jibu sahihi *D, kuunda serikali ya Jamhuri*. Bila shaka waliweza kufanya uchaguzi sahihi kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Tanzania ilipokuwa Jamhuri (1962) na lengo la mabadiliko ya Katiba lililotokana na tukio hilo.

Hata hivyo, watahiniwa wengine walichagua majibu yasiyo sahihi kama ifuatavyo: Watahiniwa 255,561 (27.87%) walivutiwa na kipotoshi *A, kuunda serikali ya umoja wa kitaifa*. Pengine watahiniwa hao walifikiri kwa kuwa Tanzania ilipata uhuru wakati huo, lengo la haraka la katiba ya 1962 lingekuwa ni kuunda serikali ya umoja wa kitaifa. Watahiniwa wengine 63,159 (6.89%) walichagua kipotoshi *B, kuunda serikali ya shirikisho*. Inawezekana watahiniwa hao walifanya chaguo hilo kutokana na kutokujua maana halisi ya neno serikali ya shirikisho ambayo ni serikali nyingi ndogondogo za kimajimbo, kwa mfano serikali ya shirikisho ya Nigeria. Watahiniwa hao huenda walifikiri kuwa, serikali ya shirikisho ni serikali

inayowashirikisha wananchi katika shughuli zake mbalimbali. Hata hivyo watahiniwa 113,710 (12.40%) walichagua kipotoshi *C, kuunda serikali za mitaa.* Watahiniwa hao hawakujua kuwa Tanzania huru haikuwa na mfumo wake wa serikali za mitaa. Watahiniwa 72,360 (7.89%) walichagua kipotoshi *E, kuunda serikali ya mpito* pengine watahiniwa hao walihusisha neno mabadiliko ya katiba lilivyotumika katika swali kuwa na maana ya serikali ya mpito.

Kwa ujumla watahiniwa walifaulu kwa wastani katika swali hili kwa sababu walikuwa na uelewa sahihi juu ya Katiba ya Jamhuri ya Tanzania ya mwaka 1962.

**Swali la 14**: Umoja wa Afrika (AU) ulianzishwa rasmi mwaka gani?


A 2002
B 2001
C 1963
D 1945
E 1999

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ushirikiano baina ya Tanzania na Mataifa Mengine*. Swali lilipima uelewa wa mtahiniwa kuhusu mwaka ambao Umoja wa Afrika ulianzishwa rasmi.

Hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya (Tazama Kielelezo Na. 6) ambapo watahiniwa 715,921 (78.08%) hawakuweza kuchagua jibu sahihi kama ifuatavyo; watahiniwa 90,313 (9.85%) walivutiwa na kipotoshi *B, 2001* kwa kuwa kilikaribiana sana na jibu sahihi. Watahiniwa wengine 381,444 (41.59%) waliochagua

kipotoshi *C, 1963* walidhani Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa Nchi huru za Afrika (OAU) ulianzishwa wakati mmoja, yaani 1963. Aidha, wapo watahiniwa 146,120 (15.93%) waliochagua kipotoshi *D, 1945* kwa kushindwa kutofautisha mwaka wa kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa (1945) na ule wa kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika (2002). Mwisho, watahiniwa (10.69%) walichagua *E, 1999* mwaka ambao haukuwa na uhusiano wowote na mwaka wa kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika. Watahiniwa hao walionesha kutokuwa na maarifa yanayotakiwa katika kujibu swali husika.

Kwa jumla ni watahiniwa 188,147 (20.52%) pekee waliochagua jibu sahihi *A, 2002*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa na taarifa sahihi na muhimu kwa ajili ya mwaka ulipoanzishwa rasmi Umoja wa Afrika (AU).




**Kielelezo Na. 6***: Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kwani asilimia 20.5tu ya watahiniwa waliweza kubaini jibu sahihi.*

Kuwepo kwa watahiniwa wengi walioshindwa kubaini jibu sahihi ni kielelezo tosha kuwa hawakuwa na uelewa sahihi wa mada husika, na hivyo hawakujua kwa uhakika mwaka wa kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika (AU).


## 2.2. Sehemu B: Historia

**Swali la 15:** Familia pana inafananishwa zaidi na kikundi jamii kiitwacho

| | |
|---|---|
| A kabila | B jamii |
| C nasaba | D jirani |
| E kijiji. | |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa katika kubaini kikundi jamii kifananacho na familia pana. Swali hili lilikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwani ni watahiniwa 302, 267 (32.96%) tu ya watahiniwa walichagua jibu sahihi *C, nasaba.* Watahiniwa hao walichagua jibu sahihi kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana na aina za familia. Uelewa wa kutosha wa watahiniwa hao, uliwawezesha kubaini kuwa nasaba ndio kikundi jamii kifananacho na familia pana kwani inajumuisha baba, mama, watoto na jamaa ambao wanaweza wakawa babu, bibi, shangazi, mjomba na wengineo ambao huweza kuja kuishi na familia (ya baba, mama na watoto) na kuifanya iwe familia pana. Aidha, jumla ya watahiniwa 602,293 (65.68%) walichagua vipotoshi *A, kabila*, *B, jamii, D, jirani* na *E, kijiji* kwa kuwa walishindwa kuelewa dhana na aina za familia. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaashiria kuwa mada ya *Familia Yetu* haikueleweka vyema kwa watahiniwa walio wengi. Kwa mfano, watahiniwa waliochagua *D, jirani* walihusianisha ukaribu na

uhusiano mwema uliopo kati ya familia moja na familia ya jirani, hivyo kudhani kuwa familia mbili zinapokaa karibu huunda familia pana. Watahiniwa 12,524 (1.4%) hawakujibu swali hili au walitoa jibu zaidi ya moja. *Kielelezo Na. 7* kinaonesha kiwango cha kufaulu katika swali hili.




**Kielelezo Na. 7** *kinaonesha kuwa ni watahiniwa wachache tu (32.96%) waliweza kubaini kikundi jamii kifananacho na familia pana.*

**Swali 16:** Mfumo wa ubugabire ulijikita katika umilikaji wa

A ng'ombe. B viwanda.

C ardhi. D Manamba.

E watumwa.

Swali lilitoka katika mada ya Kukua kwa Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala katika Jamii za Kitanzania hadi Karne ya 19. Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kubaini msingi mkuu wa ubugabire. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango hafifu

kwani, watahiniwa 289,038 (31.52%) walichagua jibu sahihi *A*, *ng'ombe*. Uelewa wa kutosha waliokuwa nao watahiwa hawa juu ya mifumo ya kiuchumi na kiutawala iliyokuwepo Afrika ya Mashariki kabla ya ukoloni, uliwawezesha kuchagua jibu sahihi. Watahiniwa hao walielewa kuwa ubugabire ulikuwa ni aina ya ukabaila ulioshamiri zaidi miongoni mwa jamii za Waha. Katika mfumo huo, mtu mwenye ng'ombe wengi (Mugabire) alimkabidhi mtu asiye na ng'ombe baadhi ya ng'ombe wake ili awatunze na baada ya kufanya kazi kwa muda fulani, yule asiye na ng'ombe (sebuja) alipewa ujira wa idadi fulani ya ng'ombe. Aidha, jumla ya watahiniwa 441,604 (48.15%) walichagua *B, viwanda* na *C, ardhi.* Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa viwanda ulikuwa msingi mkuu wa uzalishaji mali katika mfumo wa ubepari ambao haukuwepo Afrika, na ardhi ni msingi mkuu wa uzalishaji mali katika mfumo wa ukabaila ambao kwa Afrika ya Mashariki uliwakilishwa na na mfumo wa Nyarubanja.

Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaashiria kuwa baadhi ya watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya misingi mikuu ya uzalishaji mali katika mifumo mbalimbali ya kiuchumi iliyokuwepo Afrika Mashariki kabla ya ukoloni. Aidha, watahiniwa 93,490 (10.19%) walichagua *D, manamba.* Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha mifumo ya uzalishaji mali kabla na wakati wa ukoloni. Watahiniwa hao walipaswa kutambua kuwa *manamba* walikuwa ni vibarua waliokuwa wakifanya kazi za uzalishaji katika mashamba makubwa katika kipindi cha uchumi wa kikoloni. Watahiniwa 80,835 (8.81%) waliochagua *E, watumwa* walishindwa kutofautisha mifumo mbalimbali ya uzalishaji mali na misingi yake.

Kwa ujumla, uwepo wa ujumla ya watahiniwa 615,929 (67.15%) waliokosa swali hili, kunaashiria kuwa watahiniwa wengi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana za mifumo ya uzalishaji mali kabla ya ukoloni, uchumi wa kikoloni na biashara ya utumwa. Aidha, watahiniwa 12,117 (1.3%), ama hawakujibu kabisa swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja, hivyo kukosa alama.

**Swali la 17:** Mfumo wa mwanzo ambao jamii ilimiliki kwa pamoja njia kuu za uzalishaji mali uliitwa

A ukabaila.
B ukomunisti.
C ujamaa.
D urafiki.
E ujima.

Swali hili lilipima uelewa wa watahiniwa katika kubaini mfumo wa mwanzo ambao jamii ilimiliki kwa pamoja njia kuu za uzalishaji mali. Kiwango cha kufaulu katika swali hili ulikuwa wastani kwani watahiniwa 506,381 (55.22%) walichagua jibu sahihi *E, Ujima.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vipindi na sifa za mifumo mbalimbali ya uzalishaji mali. Hivyo, watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa ni katika kipindi cha ujima ambapo hakukuwa na unyonyaji na njia kuu za uzalishaji mali, kama vile ardhi na misitu zilimilikiwa na jamii nzima. Watahiniwa 159,452 (17.39%) waliochagua kipotoshi *A, Ukabaila.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini mfuatano na sifa sahihi za mifumo ya uzalishaji mali. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa ukabaila haukuwa mfumo wa kwanza wa uzalishaji mali, bali ulikuwa mfumo wa tatu uliowawezesha watu wachache kumiliki ardhi. Aidha, watahiniwa 163,580 (17.84%) walivutiwa na kipotoshi *C, Ujamaa* kwa sababu ya

kufanana kwa baadhi ya sifa za mfumo wa ujima na ujamaa. Katika Ujima njia kuu za uzalishaji mali zilimilikiwa na jamii nzima, na vivyo hivyo katika mfumo wa Ujamaa. Kwa ujumla, watahiniwa hao walipaswa kujua kuwa ujamaa haukuwa mfumo wa mwanzo wa uzalishaji mali. Kipotoshi hiki pengine kilivutia watahiniwa 163,580 (17.84%) huenda kwa sababu ya umaarufu wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea wakati wa Azimio la Arusha miaka ya 1967-1985. Kipotoshi *B, Ukomunisti* kilivutia watahiniwa 39,455 (4.30%) walioshindwa kubaini mtego wa swali. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa ukomunisti ni aina ya ujamaa ambao hauna tofauti za matabaka katika jamii na katika mfumo huu hakuna mali binafsi. Kimpangilio, ukomunisti ni mfumo wa juu zaidi wa uzalishaji mali, hivyo hauwezi kuwa mfumo wa mwanzo. Kipotoshi *D, Urafiki* ambacho kilichaguliwa na watahiniwa 36,982 (4.03%) ambao hawakuwa na uelewa kuhusu mada ya *Kukua kwa Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala katika Jamii za Tanzania* kwani urafiki haukuwa mojawapo ya mifumo ya uzalishaji mali.

**Swali la 18:** Ni mkataba upi uliharamisha biashara ya utumwa Afrika ya Mashariki mwaka 1873?

A Moresby
B Hamerton
C Berlin
D Heligoland
E Frere.

Swali lilitoka katika mada ya *Biashara ya Utumwa* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini mkataba ulioharamisha biashara ya utumwa Afrika ya Mashariki mwaka 1873. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango hafifu kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 8** kwani ni watahiniwa 218,240 tu (23.8%) walichagua


jibu sahihi *E, Frere.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa mbinu na mikataba mbalimbali waliyowekeana Waingereza na Sultani wa Zanzibar ili kukomesha biashara ya utumwa Afrika ya Mashariki.

Uwepo wa idadi kubwa ya watahiniwa 687,090 (76.20%) waliokosa swali hili kunaashiria kuwa uelewa mdogo waliokuwa nao watahiniwa kwenye mada za Biashara ya utumwa, Kuanzishwa kwa Utawala wa kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar na Kuvamiwa kwa Bara la Afrika. Kwa mfano, watahiniwa 190,491 (20.77%) waliochagua *A, Moresby* na watahiniwa 141,797 (15.46%) waliochagua *B, Hamerton* walikuwa na uelewa wa mikataba iliyotumika katika ukomeshaji wa Biashara ya utumwa katika Afrika ya Mashariki. Hata hivyo hawakuwa na uelewa wa mapungufu/mafanikio ya kila mkataba na mwaka ambao mkataba husika ulisainiwa.

Kipotoshi *C, Berlin* kilivutia watahiniwa 206,523 (22.52%) kutokana na umaarufu wa Mkutano wa Berlin katika kinyang'anyiro cha kuitawala Afrika. Mkutano huo ulifanyika kuanzia mwaka 1884-1885 huko Berlin, Ujerumani chini ya uenyekiti wa Kansela Otto von Bismarck. Kwa jumla, watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki walishindwa kutofautisha mbinu zilizotumika kuligawa Bara la Afrika na mbinu zilizotumika kukomesha biashara ya utumwa.

Watahiniwa 148,279 (16.17%) waliochagua *D, Heligoland.* Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa mkataba huu ulisainiwa mwaka 1890 baina ya Uingereza na Ujerumani. Mkataba huu uliweka mipaka baina ya Afrika Mashashariki ya Wajerumani na ile

ya Waingereza. Katika mkataba huu, Ujerumani ilikubali kubadilishana eneo la Witu nchini Kenya kwa kisiwa cha Heligoland kilichoko kaskazini mwa Ujerumani. Kimsingi, watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki walishindwa kutofautisha kati ya mikataba iliyotumika kuigawa Afrika Mashariki kati ya Waingereza na Wajerumani na mikataba iliyotumika kukomesha biashara ya utumwa katika Afrika ya Mashariki. Aidha, 1.28% ya watahiniwa hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja. Hii inashiria kuwa baadhi ya watahiniwa walikosa umakini au walishindwa kufuata maelekezo yaliyotolewa kwenye karatasi ya maswali.




**Kielelezo Na. 8** *kinaonesha ni 23.80% tu ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi kuhusu jina la mkataba ulioharamisha biashara ya utumwa Afrika ya Mashariki mwaka 1873.*

**Swali la 19:** Jumla ya taratibu zinazohusu maisha ya kila siku ya binadamu huitwa

A historia.
B utamaduni.
C desturi.
D demokrasia.
E mila.

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha neno lenye maana ya jumla ya taratibu zinazohusu maisha ya kila siku ya binadamu. Ni watahiniwa 323,274 (35.25%) tu ya watahiniwa waliweza kuchagua *B, Utamaduni* ambalo ni jibu sahihi. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya umuhimu wa vitu vinavyounda utamaduni. Watahiniwa hao walielewa kuwa utamaduni ni kioo cha jamii na unajumuisha mila, desturi, sanaa na lugha.

Idadi kubwa ya watahiniwa 265,269 (28.93%) waliovutiwa na kipotoshi *C*, *desturi* na watahiniwa 118,426 (12.91%) waliovutiwa na kipotoshi *E, mila* walishindwa kutofautisha kati ya utamaduni, desturi na mila*.* Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa desturi ni mambo ya kawaida yanayofanywa kila siku katika jamii au kikundi cha watu kama vile utii, upendo na jinsi watu wanavyosalimiana, ilhali mila ni mambo yanayofanywa na jamii fulani yanayolingana na mazingira, asili pamoja na mwenendo wa jamii hiyo.

Aidha, watahiniwa 124,724 sawa na asilimia 13.60 walichagua kipotoshi *A, Historia*. Watahiniwa hao wameonesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana za historia na utamaduni. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa historia ni elimu ya taaluma ya kumbukumbu za taarifa za matukio ya zama zilizopita ambazo

hufundishwa katika vyombo vya kielimu, na hivyo siyo jumla ya taratibu zinazohusu maisha ya kila siku ya binadamu.


Kipotoshi *D, demokrasia*, kilichaguliwa na watahiniwa 73,836 (8.05%). Inawezekana kuwa watahiniwa walivutiwa na kipotoshi hiki kutokana na ukweli kuwa dhana ya demokrasia ni mojawapo ya maswala mtambuka yanayozungumzwa sana katika vyombo vya habari kama redio, magazeti, luninga na mitandao ya kijamii. Ni wazi kuwa watahiniwa hao walikosa ufahamu wa kuelewa kuwa dhana ya demokrasia siyo taratibu zinazohusu maisha ya kila siku ya binadamu bali ni mfumo wa utawala ambao mamlaka yake yanatokana na matakwa ya umma. Vilevile, watahiniwa 12,502 (1.21%) hawakujibu swali hili na wengine waliandika jibu zaidi ya moja.

**Swali la 20:** Utandawazi umeifanya dunia kuwa kama

A nchi moja.
B wilaya.
C mpira.
D Kijiji.
E kata.

Swali liliwataka watahiniwa kubaini faida mojawapo ya utandawazi. Watahiniwa 341,150 (37.20%) walichagua jibu sahihi *D, kijiji*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha jinsi uboreshwaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano duniani ulivyorahisisha upashanaji wa habari na kuifanya dunia kuwa kama kijiji kimoja kikubwa. Yaani, jambo likitokea upande mmoja wa kijiji linafahamika kwa muda mfupi katika upande mwingine wa kijiji. Aidha, watahiniwa 425,946 (asilimia 46.44) walikosa swali hili kwa kuchagua vipotoshi *A, nchi moja* (37.31%); *B, wilaya* (6.16%), na *E, kata* (2.97%).

watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu athari ya utandawazi. Aidha, watahiniwa 137,486 (14.99%) walichagua kipotoshi *C, mpira*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki pengine ulisababishwa na uelewa mdogo waliokuwa nao kwenye mada ya utamaduni. Aidha, asilimia 1.40 ya watahiniwa ama hawakujibu au walichagua jibu zaidi ya moja hivyo kukosa alama katika swali hili kama **Kielelezo Na. 9** hapa chini kinavyoonesha.




**Kielelezo Na. 9** *kinaonesha kuwa kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango cha hafifu.*

**Swali la 21:** Umoja wa mataifa ulianzishwa mwaka


| | | | |
|---|---|---|---|
| A | 1955 | B | 1945 |
| C | 1995 | D | 1885 |
| E | 1950. | | |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ushirikiano wa Kimataifa* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini mwaka ambao Umoja wa Mataifa ulianzishwa. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa

kiwango cha wastani kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 10**. Katika swali hili, zaidi ya nusu ya watahiniwa (539,913) sawa na asilimia 58.87 walichagua jibu sahihi *B, 1945.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa dhana, chimbuko na malengo ya Umoja wa Mataifa. Watahiniwa 157,810 (17.21%) walichagua kipotoshi *C, 1995* pengine kwa sababu ya umaarufu wa mwaka huo kwani ndio ulikuwa mwaka wa kwanza kufanyika uchaguzi mkuu uliohusisha vyama vingi tokea kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini Tanzania.

Aidha, watahiniwa 115,917 (12.64%) walichagua kipotoshi *D, 1885* kutokana na kushindwa kutofautisha dhana na vipindi vya kugawanywa kwa Bara la Afrika na kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki walishindwa kuelewa kuwa mwaka 1885 ndipo ulipoisha mkutano wa kuligawa bara la Afrika uliofanyika mjini Berlin, Ujerumani, hivyo haukuwa na uhusiano wowote na kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa Umoja wa Mataifa ulianzishwa mwaka 1945 baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

Watahiniwa waliochagua vipotoshi *A, 1955* na *E, 1950* walikosa ufahamu wa kutosha katika mada ya Ushirikiano wa Kimataifa, hivyo vipotoshi hivyo havina uhusiano wowote na matakwa ya swali.




**Kielelezo Na. 10** *kinaonesha kuwa kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango cha wastani.*

**Swali la 22:** Mreno wa kwanza kufika kusini mwa Afrika aliitwa

A Mfalme Henry  B Bartholomew Diaz

C Vasco Da Gama  D David Livingstone

E Cecil Rhodes.

Swali lilitoka katika mada ya Mahusiano kati ya Jamii za Watanzania na Jamii za Asia na Ulaya na liliwataka watahiniwa kubaini jina la Mreno wa kwanza kufika kusini mwa Afrika. Swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani ni watahiniwa 292,907 (31.94%) tu ndio waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kuchagua *B, Bartholomew Diaz*. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha wa kuwa Bartholomew Diaz ndiye aliyekuwa Mreno wa kwanza kuvuka Rasi ya Tumaini Jema Cape of Good Hope hadi Mto Samaki Fish River kusini mwa Afrika mwaka 1488.

Kipotoshi *C, Vasco Da Gama* kilivuta watahiniwa 386,239 (42.12%). Watahiniwa hawa walivutiwa na kipotoshi hicho pengine kwa sababu ya umaarufu wa Vasco Da Gama katika historia ya Afrika Mashariki kwani ndiye aliyekuwa baharia na mpelelezi wa kwanza wa Kireno kufika pwani ya Afrika Mashariki na India mwaka 1498 kupitia Rasi ya Tumaini Jema, hivyo jina lake na picha zake vilikuwa bado vipo katika kumbukumbu za baadhi ya watahiniwa.

Watahiniwa 62,640 (6.83%) walichagua kipotoshi *A, Mfalme Henry*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki unaashiria kwamba baadhi ya watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu majukumu na majina ya Wareno waliofanikisha utafiti wa njia ya kwenda Asia. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa Mfalme Henry hakuwahi kufika kusini mwa Afrika bali ndiye aliyefadhili utafiti huu katika karne ya 15. Majina yaliyoko katika vipotoshi *D, David Livingstone* na *E, Cecil Rhodes* hayakuwa na uhusiano wowote na utafiti wa njia ya kwenda Asia ingawaje ni majina maarufu ya vitangulizi vya ukoloni. Pengine umaarufu wa majina haya ndilo jambo lililowavutia watahiniwa kuchagua vipotoshi vilivyokuwa na majina haya.

**Swali la 23:** Miongoni mwa sababu za kukomeshwa kwa biashara ya utumwa ni


A Huruma ya Wazungu juu ya mateso ya watumwa
B Waafrika walipigania uhuru wao
C Kupata masoko ya kuuzia bidhaa zilizotengenezwa Ulaya
D Wazungu kujali usawa wa watu wote
E Udhaifu wa watumwa kutoka Afrika.

Swali lilitoka katika mada ya Biashara ya Utumwa. Watahiniwa walitakiwa kubainisha sababu za kukomeshwa kwa biashara ya utumwa. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani ni watahiniwa 298,734 (32.57%) tu waliochagua jibu sahihi *C, Kupata masoko ya kuuzia bidhaa zilizotengenezwa Ulaya.* Watahiniwa hao walielewa kuwa mageuzi makubwa ya viwanda yaliyoyotokea huko Ulaya katika karne ya 18 na 19 yalisababisha kuongezeka kwa mahitaji ya malighafi na masoko, hivyo Waafrika walitakiwa wabaki katika nchi zao ili wazalishe malighafi au wawe soko la bidhaa za viwandani kutoka Ulaya. Kwa ujumla, watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha wa dhana ya utumwa, chimbuko, athari na sababu za kukomeshwa kwa biashara hiyo. **Kielelezo Na. 11** kinaonyesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.

Watahiniwa 395,939 (43.17%) walivutiwa na kipotoshi *B, Waafrika walipigania uhuru wao.* Hii imesababishwa na uelewa mdogo wa watahiniwa kushindwa kutofautisha mada ya utumwa na harakati za kupigania uhuru katika Afrika ambazo zilianza baada ya kushamiri kwa utawala wa kikoloni. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa utumwa uliisha mwishoni mwa karne ya 19 ilhali harakati za kupigania uhuru zilianza baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

Vipotoshi *A, huruma ya Wazungu juu ya mateso ya watumwa* na *D, Wazungu kujali usawa wa watu wote* vilichaguliwa na watahiniwa ambao walikuwa na uelewa mdogo juu ya chimbuko na kukua kwa biashara ya utumwa. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa biashara hii ilianzishwa na kufanywa na Wazungu, hivyo kama (wazungu) wangekuwa na huruma na kujali usawa wa watu wote

wasingeanzisha wala kujihusisha katika biashara hii iliyomdhalilisha mwanadamu kwa kiwango kikubwa. Yawezekana pia, kuwa huenda jitihada kubwa na mbinu zilizofanywa na Wazungu katika karne ya 19 za kukomesha biashara hii ziliwavuta baadhi ya watahiniwa ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha kudhani kuwa utu uliwafanya wazungu kuyatambua na kuyazuia mateso waliyokuwa wakiyapata watumwa. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa kama wazungu wangekuwa na utu na kama biashara hii isingekuwa na faida ya kiuchumi kwao basi wasingekaa kimya muda mrefu hivi (miaka 400) bila kuikomesha. Aidha, watahiniwa 69,130 (7.54%) waliochagua E, *Udhaifu wa watumwa kutoka Afrika*, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sababu za Waafrika kupelekwa utumwani na sababu za kukomeshwa kwa biashara ya utumwa. Biashara ya utumwa ilikomeshwa kutokana na mageuzi ya kiviwanda yaliyoleta mabadiliko makubwa ya uzalishaji katika sekta za kilimo, viwanda na usafirishaji. Hivyo, iliwalazimisha mabepari wa kizungu kukomesha biashara ya watumwa ili kuwezesha upatikanaji wa malighafi na masoko Afrika kwa urahisi. Aidha, watahiniwa 11,973 (1.30%) hawakujibu kabisa swali hili na wengine walichagua jibu zaidi ya moja.




**Kielelezo Na. 11** *kinaonesha kuwa watahiniwa walifaulu kwa kiwango hafifu (32.57%) katika swali hili.*

**Swali la 24:** Makundi makuu ya vitangulizi vya ukoloni yaliyokuja Tanganyika na Zanzibar yalikuwa

A askari, wamisionari na watawala

B wamisionari, waandishi wa habari na wafanyabiashara


C wapelelezi, watawala na wafanyabiashara

D waandishi wa habari, wapelelezi na askari

E wapelelezi, wamisionari na wafanyabiashara.

Swali hili lilitoka katika mada ya Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika na Zanzibar. Swali lilipima uelewa wa watahiniwa katika kubaini makundi ya vitangulizi vya ukoloni yaliyokuja Tanganyika na Zanzibar. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa ni kwa kiwango kizuri kwani watahiniwa 679, 477 (74.09%) walichagua jibu sahihi *E wapelelezi, wamisionari na wafanyabiashara* (Angalia **Kielelezo Na. 12)**. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa maarifa

ya kutosha kuhusu dhana za ukoloni na makundi wakilishi ya wakoloni yaliyokuja nchini kutoka Ulaya katika karne ya 19 ili kufanikisha maslahi yao ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hata hivyo, watahiniwa 224,549 (24.49%) walikosa swali hili kwa kuchagua vipotoshi *A, askari, wamisionari na watawala*; *B*, *wamisionari, waandishi wa habari na wafanyabiashara; C*, *wapelelezi, watawala na wafanyabiashara* na *D, waandishi wa habari, wapelelezi na askari*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walishindwa kuelewa kuwa waandishi wa habari, watawala na askari hawakuwa sehemu ya makundi ya vitangulizi vya ukoloni. Kwa ujumla, watahiniwa hao walishindwa kutofautisha majukumu ya makundi mbalimbali kabla na wakati wa ukoloni. Kwa mfano, watawala na askari hawakuwa sehemu ya vitangulizi vya ukoloni lakini walifanya kazi kubwa wakati wa uvamizi na utawala wa kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaweza kuwa umechangiwa na umaarufu wa mbinu hizo katika uvamizi wa kikoloni katika Afrika Mashariki. Jumla ya watahiniwa 13,058 (1.4%) hawakujibu swali hili au walitoa jibu zaidi ya moja.




**Kielelezo Na. 12** *kinaonesha kufaulu kwa kiwango kizuri (74.1%) kwa watahiniwa waliofanya swali hili.*

**Swali la 25:** Mkataba wa mwaka 1890 ulioigawa Afrika Mashariki kwa Wajerumani na Waingereza ulijulikana kama

A Mkataba wa Hamerton

B Mkataba wa Heligoland

C Mkataba wa Moresby

D Mkataba wa Afrika Mashariki

E Mkataba wa Frere.

Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la mkataba ambao uliigawa Afrika Mashariki kwa Wajerumani na Waingereza mwaka 1890. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 435,447 (47.48%) walichagua jibu sahihi *B, Mkataba wa Heligoland*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mbinu na majina ya mikataba iliyotumika kuigawa Afrika Mashariki kati ya Wajerumani na Waingereza. Hata hivyo, watahiniwa 335,756

(36.62%) walichagua vipotoshi *A, Mkataba wa Hamerton; C, Mkataba wa Moresby* na *E, Mkataba wa Frere.* Watahiniwa hao walichagua majina ya mikataba iliyotumika katika ukomeshaji wa biashara ya watumwa katika Afrika ya Mashariki. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unadhihirisha uelewa mdogo waliokuwa nao baadhi ya watahiniwa katika mada za Biashara ya Watumwa na Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika. Kwa ujumla watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kati ya mikataba iliyosainiwa kukomesha biashara ya watumwa Afrika ya Mashariki na mikataba iliyotumika kuigawa Afrika ya Mashariki kati ya Wajerumani na Waingereza.

Asilimia 14.59 ya watahiniwa waliovutwa na kipotoshi *D, Mkataba wa Afrika Mashariki* hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya ukoloni na mbinu walizotumia Wajerumani na Waingereza kuigawa Afrika ya Mashariki. Pengine, uwepo wa maneno Afrika Mashariki kwenye mzizi wa swali na kwenye kipotoshi ndio kilikuwa chambo kilichowanasa watahiniwa waliokuwa hawajajiandaa vema. Pamoja na hayo, uwepo wa watahiniwa 9,826 (1.10%) ambao hawakufanya swali hili na watahiniwa 2,260 (0.20%) ambao walichagua jibu zaidi ya moja ni ushahidi kuwa baadhi ya watahiniwa walikosa maarifa na ujuzi wa kutosha katika mada iliyotahiniwa na kufuata maelekezo ya mtihani.

**Swali la 26:** Baadhi ya yaliyokuwa makoloni ya Ufaransa katika Bara la Afrika ni

A Togo na Moroko
B Senegali na Ghana
C Naijeria na Tunisia
D Senegali na Moroko
E Angola na Tunisia.

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini yaliyokuwa makoloni ya Ufaransa katika Bara la Afrika. Swali hili lilikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwani ni watahiniwa 200,797 (21.9%) waliochagua jibu sahihi *D, Senegali na Moroko.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya mgawanyo wa Bara la Afrika baada ya mkutano wa Berlin wa mwaka 1884-1885.

Hata hivyo, watahiniwa 701,944 (76.54%) walikosa swali hili kwa kuchagua vipotoshi *A*, *Togo na Moroko*; *B, Senegali na Ghana*; *C, Naijeria na Tunisia* na *E, Angola na Tunisia*. Kwa ujumla, watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa baadhi ya vipotoshi vilikuwa na nchi ambazo hazikuwa makoloni ya Ufaransa. Kwa mfano, Naijeria na Ghana zilikuwa ni makoloni ya Uingereza, ilhali Angola ilikuwa koloni la Ureno. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaonesha watahiniwa wengi hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada za Uvamizi wa Kimataifa na Kuvamiwa kwa Bara la Afrika. Aidha, jumla ya watahiniwa 14,343 (1.60%), ama hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 27:** Kiongozi wa Bunyoro aliyeongoza watu wake kupigana na Waingereza nchini Uganda ni


A Kabaka Mwanga B Kabalega
C Lobengula D Lewanika
E Samori Toure.

Katika swali hili, watahiniwa walipimwa ufahamu wao katika kubaini jina la kiongozi wa Bunyoro aliyeongoza watu wake kupigana na Waingereza nchini Uganda. Hili ni mojawapo ya maswali yaliyokuwa

na kiwango hafifu cha kufaulu katika somo hili kwani ni watahiniwa 178,028 (19.41%) tu waliochagua jibu sahihi *B, Kabalega* kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 13, Hii inaashiria kuwa watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha juu ya mbinu zilizotumiwa na Waafrika kupinga uvamizi wa wakoloni. Watahiniwa hao walielewa kuwa Wabunyoro chini ya uongozi wa Omukama Kabalega waliwapinga kwa njia ya vita wakoloni wa Kiingereza mwaka 1872. Aidha, watahiniwa 379,273 (41.36%) walivutiwa na kipotoshi *A, Kabaka Mwanga* pengine kutokana na umaarufu wa jina Kabaka na dola ya Buganda kwa jumla miongoni mwa watahiniwa.

Aidha, vipotoshi *C, Lobengula* na *E, Samori Toure* vilichaguliwa na watahiniwa 257,590 (28.09%) ambao kwa upande mmoja walikuwa na uelewa wa viongozi waliopinga uvamizi wa kikoloni kwa njia ya vita, ingawa kwa upande mwingine walishindwa kubaini kuwa Lobengula na Samori Toure hawakuwa viongozi wa Wabunyoro bali walikuwa ni viongozi Wandebele na Wamandika mtawalia.

Kipotoshi *D*, Lewanika, kilivutia watahiniwa 88,912 (9.70%). Kipotoshi hiki kilichaguliwa na watahiniwa walioshindwa kubaini kuwa Lewanika hakuwa kiongozi wa Bunyoro bali alikuwa kiongozi wa Dola ya Lozi ambaye hakupigana na Waingereza bali alishirikiana nao ili wamsaidie vita dhidi ya Wandebele waliokuwa chini ya Lobengula. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaashiria kuwa baadhi ya watahiniwa hawakuzielewa vema dola za Kiafrika na majina ya viongozi wake waliopinga ukoloni kwa njia ya vita au kwa njia ya makubaliano. Watahiniwa 10,655 (1.10%) hawakujibu swali hili na watahiniwa 2,616 (0.30%) walichagua jibu zaidi ya moja.




***Kielelezo Na. 13*** *kinaonesha ufaulu hafifu katika swali hili, kwani ni watahiniwa (19.41%) tu waliweza kuchagua jibu sahihi.*

**Swali la 28:** Azimio la Arusha lilisisitiza kuwa maendeleo ya nchi lazima yapatikane katika misingi ya

A Utegemezi na misaada

B Biashara za kimataifa

C Ujamaa na kujitegemea

D Chama kimoja na demokrasia

E Ubinafsishaji na uwekezaji.

Swali hili liliwataka watahiniwa kubaini misingi ya upatikanaji wa maendeleo ya nchi kwa mujibu wa Azimio la Arusha. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani zaidi ya nusu ya watahiniwa, yaani 543,894 (59.31%) walichagua jibu sahihi *C, Ujamaa na Kujitegemea*. Watahiniwa hao walichagua jibu sahihi kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya Mabadiliko

ya Kiuchumi katika Tanzania Huru. Watahiniwa asilimia 7.03 waliochagua kipotoshi *A, Utegemezi na misaada* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mambo yanayokwamisha maendeleo katika nchi za Kiafrika. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa utegemezi wa misaada ndilo jambo ambalo limekuwa likisababisha kuyumba kwa uchumi wa nchi nyingi za Kiafrika kutokana na madeni makubwa ya nje yaliyotokana na mikopo yenye riba kubwa.

Aidha, kipotoshi *B, Biashara za kimataifa* kilivuta watahiniwa 108,198 (11.8%). Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa biashara za kimataifa ndizo zilikuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo ya Tanzania kutokana na malighafi zitokazo Tanzania kuuzwa kwa bei ndogo katika soko la dunia ikilinganishwa na mashine au vipuli kutoka Ulaya. Hivyo, watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu hatua zilizochukuliwa na nchi za Kiafrika kujikwamua kiuchumi.

Watahiniwa waliochagua kipotoshi *D, Chama kimoja na demokrasia* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu malengo ya Azimio la Arusha. Kwa kiwango kikubwa, inaelekea watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kati ya dhana za kiuchumi na kisiasa zilizoambatana na mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi nchini Tanzania kuanzia mwaka 1965.

Watahiniwa 79,274 (8.64%) walivutiwa na kipotoshi *E, Ubinafsishaji na uwekezaji* pengine kwa sababu ya umaarufu wa sera ya ubinafsishaji na uwekezaji. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa uchumi wa soko huria haukuwa mojawapo ya misingi ya

Azimio la Arusha. Kwa ujumla, mwelekeo wa chaguzi hizo zisizo sahihi unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa walikuwa na uelewa hafifu katika dhana za Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya Siasa nchini Tanzania na utandawazi. Watahiniwa ambao hawakufanya swali ni 9,992 (1.10%) na watahiniwa 2,403 (0.30%) walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 29:** Tanzania iliingia katika mfumo wa vyama vingi kwa mara ya pili mwaka

A 1995 B 1992

C 1963 D 1985

E 1965.

Swali hili lilitoka katika mada ya Mabadiliko ya Kiuchumi katika Tanzania Huru. Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha mwaka ambao Tanzania iliingia katika mfumo wa vyama vingi kwa mara ya pili. Swali lilikuwa na kiwango cha kufaulu cha wastani kwani watahiniwa 457,422 sawa na asilimia 49.88 walichagua jibu sahihi *B, 1992.* Watahiniwa waliochagua jibu sahihi walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu mada ya *Mabadiliko ya Kisiasa katika Tanzania Huru.* Watahiniwa hao walielewa kuwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini Tanzania ulirejeshwa na Tume iliyoongozwa na Francis Nyalali (maarufu kama tume ya Nyalali mwaka 1992).

Kipotoshi *A, 1995* kilivuta watahiniwa 210,149 (22.91%) kwa sababu watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kati ya mwaka ambao mfumo wa vyama vingi vya siasa ulirejeshwa nchini Tanzania na mwaka ambao uchaguzi mkuu wa kwanza tokea kurejeshwa kwa

mfumo wa vyama vingi nchini Tanzania ulifanyika. Watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa mwaka 1995 ndio ulikuwa mwaka wa kwanza kufanyika uchaguzi mkuu unaohusisha vyama vingi vya siasa tokea kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini Tanzania.

Watahiniwa 111,602 (12.17%) walivutiwa na kipotoshi *C, 1963.* Kipotoshi hicho hakikuwa na uhusiano na matakwa ya swali. Pengine kilichaguliwa kutokana na uchaguzi uliofanyika mwaka huo ambapo chama cha Afro Shiraz Party kilishinda ingawa hakikupewa nafasi ya kuunda serikali. Kinyume chake, Waingereza waliwapa Waarabu nafasi hiyo kupitia chama cha Zanzibar Nationalist Party (ZNP) na Zanzibar and Pemba People’s Party (ZPPP).

Aidha, baadhi ya watahiniwa walichagua kipotoshi *D, 1985* pengine kutokana na umaarufu wa wake katika siasa na uchumi wa Tanzania. Huu ndio mwaka ambao Rais Ali Hassan Mwinyi aliruhusu uchumi wa Tanzania kufuata mfumo wa soko huria.

Watahiniwa waliochagua kipotoshi *E, 1965* walikuwa na uelewa wa dhana ya vyama vingi ingawa walishindwa kutofautisha kati ya mwaka (1965) ambao vyama vingi vilipigwa marufuku na mwaka (1992) ambao vilirejeshwa nchini Tanzania. Uchaguzi wa vipotoshi hivi kwa jumla unaashiria kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kuhusu matukio muhimu ya kisiasa yaliyotokea nchini kuanzia mwaka 1961. Watahiniwa 9,969 (1.09%) hawakufanya swali hili ambapo watahiniwa (2,397) 0.30% walichagua jibu zaidi ya moja.

Jambo hili linaashiria kwamba baadhi ya watahiniwa hawafuati maelekezo ya mtihani.

**Swali la 30:** Ni ipi ni faida ya kuwa na chama kimoja cha siasa?

A Huwafanya baadhi ya viongozi wa Kiafrika kuwa madikteta.

B Huwafanya wananchi kuwa na uhuru wa kujieleza.


C Hutoa wigo kwa watu wengi kushiriki shughuli za kisiasa

D Hupunguza migogoro itokanayo na tofauti za kiitikadi

E Huwawezesha wananchi kuikosoa serikali yao wakati wowote.

Swali hili liliwataka watahiniwa kubaini faida ya kuwa na chama kimoja cha siasa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 390,495 (42.58) walichagua jibu sahihi *D, Hupunguza migogoro itokanayo na tofauti za kiitikadi* kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 14**. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha katika mada ya *Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru.* Kwa ujumla, watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu faida na hasara za mfumo wa chama kimoja au vyama vingi vya siasa katika nchi, hivyo ilikuwa rahisi kwao kubaini jibu sahihi kutoka kwenye chaguzi walizopewa. Uchaguzi wa jibu sahihi, huenda pia ukawa umesababishwa na uzoefu waliokuwanao watahiniwa kupitia vyombo vya habari kama redio, runinga (*television*) na magazeti pamoja na mitandao ya kijamii kushuhudia mivutano ya kisiasa bungeni au katika mikutano ya hadhara sehemu mbalimbali nchini na nchi za nje.

Watahiniwa 512,614 walichagua vipotoshi katika uwiano ufuatao; *A, Huwafanya baadhi ya viongozi wa Kiafrika kuwa madikteta (12.57%); B, Huwafanya wananchi kuwa na uhuru wa kujieleza (17.00%)*; *C, Hutoa wigo kwa watu wengi kushiriki shughuli za kisiasa (14.8%) na E, Huwawezesha wananchi kuikosoa serikali yao wakati wote (11.49%). Kiuhalisia, vipotoshi hivyo* vilivuta idadi inayokaribiana ya watahiniwa. Kukaribiana kwa asilimia katika vipotoshi hivyo, kunadhihirisha kuwa watahiniwa wengi hawakuwa na maarifa ya kutosha kutofautisha kati ya faida au hasara za mfumo wa chama kimoja cha siasa na ule mfumo wa vyama vingi vya siasa. Watahiniwa 13,975 (1.5%) hawakujibu swali hili na wengine walichagua jibu zaidi ya moja.




**Kielelezo Na. 14** *kinaonesha kuwa asilimia 42.6 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi na hivyo kufaulu kwao kulikuwa ni kwa kiwango cha wastani.*

**Swali la 31:** Ipi sio kweli kuhusu sifa za elimu iliyotolewa Tanzania kabla ya uhuru?

A Ilitolewa kwa watu wote.

B Ilibagua watoto wa kike.

C Ilikuwa ya matabaka

D Ilikuwa ya nadharia kuliko vitendo

E Ilitolewa kwa misingi ya kidini.

Katika swali hili, watahiniwa walitakiwa kubainisha sifa ambayo haikuendana na elimu iliyotolewa Tanzania kabla ya uhuru. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa ni kwa kiwango cha wastani. Hii inamaanisha kwamba ni watahiniwa 411,152 (44.83%) waliochagua jibu sahihi *A, ilitolewa kwa watu wote*.

Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya elimu iliyotolewa wakati wa ukoloni. Kwa hiyo walibaini kuwa elimu ya kipindi hicho ilikuwa ni ya kibaguzi na haikutolewa kwa watu wote.

Idadi kubwa ya watahiniwa 204,487 (22.30%) walivutiwa na kipotoshi *B, Ilibagua watoto wa kike*. Kipotoshi hiki kilichaguliwa na watahiniwa wengi pengine kutokana na watahiniwa kukosa umakini katika kubaini matakwa ya swali. Sentensi ilibagua watoto wa kike ilikuwa ni sifa inayoendana na elimu iliyotolewa wakati wa ukoloni kinyume na matakwa ya swali yaliyohitaji sifa ambayo haikuendana na elimu hiyo. Huenda, pia kipotoshi hiki kilivutia watahiniwa wengi kutokana na msisitizo uliowekwa miaka ya hivi karibuni na serikali kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike.

Vipotoshi *C, Ilikuwa ya matabaka; D, Ilikuwa ya nadharia kuliko vitendo* na *E, Ilitolewa kwa misingi ya kidini* vilichaguliwa na

watahiniwa ambao walishindwa kubaini matakwa ya swali. Swali liliwataka kubaini sifa ambayo haikuendana na elimu iliyotolewa kabla ya uhuru lakini wao wakachagua vipotoshi vyenye sifa ya elimu kabla ya uhuru. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unashiria mambo mawili: Jambo la kwanza ni kuwa zaidi ya nusu ya watahiniwa 493,378 (53.70%) hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu huduma za jamii wakati wa ukoloni, au watahiniwa hawakuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha katika kubaini matakwa ya swali. Watahiniwa 16,286 (1.8%), ama hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 32:** Urejeshwaji wa mfumo wa vyama vingi Tanzania ulipendekezwa na

A Tume ya Kisanga
B Tume ya Nyalali
C Tume ya Makweta
D Tume ya Karume
E Tume ya Warioba.

Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kubaini jina la tume iliyopendekeza urejeshwaji wa mfumo wa vyama vingi nchini Tanzania. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu pamoja na kwamba dhana ya vyama vingi ni maarufu miongoni mwa watahiniwa. Watahiniwa 233,856 (25.50%) waliweza kuchagua jibu sahihi *B, Tume ya Nyalali.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu hatua zilizochukuliwa na serikali katika kurejesha mfumo wa vyama vingi ikiwa ni pamoja na kuunda tume (Tume ya Nyalali) iliyoratibu maoni ya wananchi na kuleta mapendekezo ambayo yalihalalisha mfumo wa vyama vingi nchini mwaka 1992.

Aidha, watahiniwa 351,932 (38.4%) walivutiwa na kipotoshi *D, Tume ya Karume* pengine kwa sababu ya umaarufu wa familia ya Karume katika historia ya Tanzania (Abeid Aman Karume na mwanaye Aman Karume waliowahi kuwa Marais wa Zanzibar na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) katika masuala ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar au maridhiano kati ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na Civil United Front (CUF) yaliyoleta Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar. Watahiniwa hao walitakiwa kuelewa kuwa Karume hajawahi kuongoza tume yoyote iliyoratibu maoni ya wananchi kuhusu urejeshwaji wa mfumo wa vyama vingi katika Tanzania.

Aidha, watahiniwa 315,010 (35%) waliochagua vipotoshi *A, Tume ya Kisanga; C, Tume ya Makweta;* na *E, Tume ya Warioba* walikuwa na uelewa wa majina ya watu waliowahi kuongoza tume mbalimbali ingawa walishindwa kuoanisha jina la mhusika na tume aliyoiongoza. Kwa ujumla watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa tume ya Kisanga ilihusika na mambo yaliyohusu Haki za Binadamu; tume ya Makweta ilihusika na mambo yaliyohusu Elimu, ilhali tume ya Warioba ilihusika na mambo yanayohusu Katiba mpya. Hivyo, katika muktadha huu, inaonekana watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu madhumuni ya tume mbambali ambazo zilishawahi kuundwa nchini Tanzania. Watahiniwa 16,286 (1.7%) hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.


### 2:3 Sehemu C: Jiografia

**Swali la 33:** Mazingira ni

- A viumbe hai na visivyo hai
- B viumbe hai, nyumba na maji
- C vitu vyote vinavyomzunguka binadamu
- D ardhi, majengo na bahari
- E mimea, wanyama wafugwao na nyumba.

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kubainisha maana ya neno mazingira. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa umeoneshwa katika **Kielelezo Na. 15**. Watahiniwa 776,380 (84.70%) waliweza kuchagua jibu sahihi *C, vitu vyote vinavyomzunguka binadamu.* Watahiniwa hawa waliweza kubaini kwa urahisi maana ya neno mazingira kwa sababu ndiyo sehemu ya maisha yao ya kila siku.

Watahiniwa 130,360 (14.2%) walichagua kati ya vipotoshi *A, viumbe hai na visivyo hai, B, viumbe hai, nyumba na maji, D, ardhi, majengo na bahari na E, mimea, wanyama wafugwao na wa nyumbani.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa chaguo hizo ni sehemu ya vitu vinavyounda mazingira, hivyo haviwezi kusimama peke yake. Aidha, watahiniwa 10,344 (1.1%) hawakujibu swali hili.




**Kielelezo Na. 15:** *kinafafanua takwimu za majibu ya watahiniwa katika swali la 33 ambapo kufaulu kwa watahiniwa ni kwa kiwango kizuri (84.66%).*

**Swali la 34:** Matumizi sahihi ya mistari ya gridi katika ramani ni

A kutafuta mahali
B kuonyesha uelekeo wa mashariki
C kuonyesha umbali
D kutafuta wakati
E kuonyesha uelekeo wa kaskazini.

Swali hili lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu stadi sahili za ramani, hasa katika kipengele cha matumizi ya mistari ya gridi katika ramani. Jumla ya watahiniwa 468,876 (51.13%) walijibu kwa usahihi swali hili kwa kuchagua *A, kutafuta mahali.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa mistari ya gridi inatumika kutafuta mahali katika ramani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 85,504 (9.32%), waliochagua kipotoshi *B, kuonyesha uelekeo wa mashariki.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa mistari ya gridi haitumiki kuonyesha uelekeo wa mashariki katika ramani. Jumla ya watahiniwa 196,405, sawa na asilimia 21.42, waliochagua kipotoshi *C, kuonyesha umbali,* walishindwa kutambua kuwa rula, bikari, uzi, ncha ya karatasi na uelekeo hutumika kukokotoa umbali katika ramani sambamba na matumizi ya skeli. Watahiniwa 89,886, (9.80%), walichagua kipotoshi *D, kutafuta wakati,* walishindwa kubaini kuwa mistari ya longitudo ndiyo ambayo hutumika kutafuta wakati. Watahiniwa 64,228, (7.00%), walichagua kipotoshi *E, kuonyesha uelekeo wa kaskazini.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa uelekeo wa kaskazini katika ramani huoneshwa kwa kutumia dira. Uchaguzi wa vipotoshi hivi ni ishara kuwa mada ya usomaji wa ramani haikueleweka vizuri kwa watahiniwa wengi. Watahiniwa 12,185, (1.30%), hawakujibu swali hili.

**Swali la 35**: Chanzo kikuu cha mfumo wa jua ni

A Dunia
B Sayari
C Jua
D Mwezi
E Nyota.

Swali lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kubaini chanzo kikuu cha mfumo wa jua. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili hakukuwa kwa kuridhisha kwani ni watahiniwa 183,301 (19.99%) tu ambao ni pungufu ya robo ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, waliweza kuchagua jibu sahihi *C, jua*. Watahiniwa hao wachache walikuwa na ufahamu wa mfumo wa jua kwani jua ndilo mhimili mkuu na sayari zote zinalizunguka jua.

Watahiniwa wengi 403,385 (43.99%) walivutiwa na chaguo *B sayari*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki kunaonesha wazi kuwa watahiniwa walishindwa kutofautisha jua na sayari pamoja na ukweli kuwa vyote vinajumuisha mfumo wa jua. Aidha, watahiniwa 136,783 (14.91%), waliochagua *A*, *Dunia*, watahiniwa 72,384 (7.89%) waliochagua *D, Mwezi* pamoja na watahiniwa 110,189 (12.02%) waliochagua *E, Nyota kwa kuwa* walishindwa kutofautisha Jua kama nyota ambayo ndiyo chanzo kikuu cha nishati katika mfumo wa jua pamoja na Mwezi na Nyota nyingine nje ya mfumo wa jua. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ni kielelezo cha ufinyu wa maarifa waliokuwa nao watahiniwa, hasa kuhusu unajimu. Aidha watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuwa jua ni mhimili wa mfumo wa jua na sayari zote zinalizunguka. Hata hivyo, watahiniwa 11,042 (1.20%), hawakujibu swali hili.


**Swali la 36:** Vifuatavyo ni vyanzo vya maji isipokuwa

A visima B chemichemi
C mito D mabomba
E maziwa.

Swali hili lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa kuhusu vyanzo vya maji. Uchambuzi wa kufaulu katika swali hili unaonesha kuwa mzuri kwani watahiniwa 601,097 (65.54%) walichagua *D*, *Mabomba* ambalo ni jibu sahihi. Kiwango hiki cha kufaulu kinaonesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa vyanzo vya maji na umuhimu wa maji katika shughuli za kila siku za binadamu. Pia, walikuwa na uelewa kuwa mabomba ni njia ya kupitia maji yanayotoka katika vyanzo mbalimbali vya maji kama chemichemi, mito, visima na maziwa.

Watahiniwa wengine 53,999 (5.89%) walichagua *A, visima;* watahiniwa 123,763 (13.50%) walichagua *B, chemichemi;*

watahiniwa 40,591 (4.43%) walichagua *C, mito* na watahiniwa 86,411 (9.42%) walichagua *E, maziwa*. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi *A, B, C,* na *E* walishindwa kutofautisha kati ya vyanzo vya maji na njia za kusambaza maji ili yawafikie watumiaji. Aidha, watahiniwa 11,223, sawa na asilimia 1.20, hawakufanya swali hili. Ufafanuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa umetolewa katika Kielelezo Na. 2.16 hapa chini.




**Kielelezo Na. 2.16:** *kinafafanua takwimu za majibu ya watahiniwa katika kila chaguo ambazo zinaonesha kiwango kizuri cha kufaulu.*

**Swali la 37:** Uchafuzi wa hewa kwenye makazi ya watu unaweza kudhibitiwa kwa

A kutumia vyoo
B kuchoma taka
C kutiririsha maji taka mitaani
D kuchemsha maji ya kunywa
E kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki.

Swali hili lilipima uwezo wa mtahiniwa kubaini njia mbalimbali zinazotumika kudhibiti uchafuzi wa hewa katika makazi ya watu.

Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa hafifu sana kwani ni watahiniwa 184,833 tu, (20.15%), waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni *A, kutumia vyoo*. Kiwango hiki cha kufaulu kinaashiria kuwa ni watahiniwa wachache tu walikuwa na uelewa wa kutokomeza hewa chafu kwenye makazi ya watu.

Watahiniwa 318,606 (34.74%) waliochagua kipotoshi *B, kuchoma taka* walishindwa kubaini kuwa uchomaji wa taka unasababisha uchafuzi wa hewa badala ya kudhibiti uchafuzi wa hewa. Watahiniwa 103,077 (11.24%) walivutiwa na kipotoshi *C*, *Kutiririsha maji taka mitaani* kutokana na kukosa uelewa wa uchafuzi wa hewa unaotokana na ukosefu wa vyoo katika makazi ya watu. Watahiniwa 57,278, sawa na asilimia 6.25, walichagua kipotoshi *D, kuchemsha maji ya kunywa.* Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kuchemsha maji ya kunywa kama njia ya kuepukana na magonjwa yanayotokana na matumizi ya maji yasiyo salama na uchafunzi wa hewa. Kwa upande mwingine, watahiniwa 240,388 (26.21%) walichagua kipotoshi *E, kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa matumizi ya mifuko ya plastiki husababisha uchafuzi wa udongo na siyo uchafuzi wa hewa. Aidha, matumizi ya mifuko ya plastiki huchafua hewa pale ambapo itachomwa moto. Watahiniwa 12,902 (1.40%) hawakujibu swali hili.

**Swali la 38:** Pitio ni eneo la uso wa ardhi linalooonesha

A sehemu yenye Bonde la Ufa
B sehemu yenye mlima tofali
C sehemu iliyoko juu ya vilele vya milima
D eneo tambarare
E sehemu ya wazi kati ya vilele viwili vya milima.

Swali hili lilikusudia kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu maumbo ya asili yanayopatikana katika uso wa dunia. Pia, lilipima uwezo wa mtahiniwa kutofautisha muonekano wa umbo la pitio na maumbo mengine ya asili yanayopatikana katika uso wa dunia. Kwa ujumla kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa wastani kwani ni jumla ya watahiniwa 461,247 (50.29%) walioweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni *E, sehemu ya wazi kati ya vilele viwili vya milima.* Uchaguzi wa jibu hili sahihi unaonesha kuwa watahiniwa walio wengi walikuwa wanaweza kutofautisha muonekano wa maumbo mbalimbali yanayopatikana katika uso wa dunia hasa muonekano wa pitio na maumbo mengine.

Watahiniwa wengine walishindwa kuchagua jibu sahihi kutokana na kuwa na uelewa mdogo wa namna pitio linavyoumbwa. Jumla ya watahiniwa 128,999 (14.07%), walichagua kipotoshi *A, sehemu ya bonde la ufa.* Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha mwonekano wa Bonde la Ufa na ule wa pitio. Watahiniwa 54,072 (5.90%) waliochagua kipotoshi *B*, *sehemu yenye mlima tofali* walishindwa kutambua kuwa pitio hutengenezwa katikati ya safu ya milima mikunjo na sio milima tofali. Kundi la watahiniwa 123,282 (13.44%) waliochagua *C*, *sehemu iliyo juu ya vilele vya milima* walishindwa kubaini kuwa pitio ni sehemu ya bonde hivyo ni tofauti na sehemu za juu ya milima. Aidha, watahiniwa 136,491 (14.88%), waliochagua kipotoshi *D, eneo tambarare* walishindwa kubaini kuwa pitio hufanyika katikati ya eneo lenye mwinuko na sio tambarare. Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 12,993 (1.40%), hawakujibu swali hili.

**Swali la 39:** Tafuta umbali halisi katika kilometa kati ya eneo R na S ikiwa umbali katika ramani ni sentimeta 15 na kipimio cha ramani ni: 1:100,000.

A km 50
B km 0.15
C km 100,000
D km 7.5
E km 15.

Swali hili lilipima uwezo wa mtahiniwa kutumia kwa usahihi njia mbalimbali za kuwasilisha vipimio na kubadili vipimio kutoka katika njia moja kwenda nyingine. Watahiniwa walitegemewa kuonyesha ujuzi wao katika kubadili umbali katika ramani kuwa umbali halisi wa eneo katika ardhi katika kilomita. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa hafifu kwani ni watahiniwa 248,896 (27.14%) waliweza kuchagua *E*, *Km 15* ambalo ni jibu sahihi. Watahiniwa hao walikuwa na ujuzi wa namna ya kukokotoa umbali katika ramani na kwenda kuwa umbali halisi wa eneo katika ardhi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 220,869 (24.08%) waliochagua kipotoshi *B*, *Km 0.15*, walionesha kutofahamu namna ya kubadilisha urefu katika ramani kuwa umbali halisi katika ardhi. Vilevile watahiniwa 176,859 (19.28%) walichagua kipotoshi *C*, *Km 100,000*. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kubadili umbali katika ramani kwenda umbali halisi katika ardhi, lakini pia walivutiwa na namba za kipimio cha ramani (100,000) kama zinavyoonekana katika swali husika.

Watahiniwa wengine 252,833 (27.57%) walichagua vipotoshi *A*, *Km 50* na *D*, *Km 7.5* ambavyo havina uhusiano kabisa na swali. Watahiniwa 17,624 (1.90%) hawakujibu swali hili.


**Swali la 40**: Mikoa inayolima ndizi nchini Tanzania ni

A Kagera, Kilimanjaro na Mbeya
B Mbeya, Kagera na Lindi
C Kagera, Singida na Shinyanga
D Arusha, Morogoro na Shinyanga
E Singida, Lindi na Kagera.

Swali hili lililenga kupima ufahamu wa watahiniwa kuhusu mazao yanayozalishwa katika mikoa mbalimbali nchini Tanzania. Ili watahiniwa waweze kujibu vema swali hili, walitakiwa kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mikoa mbalimbali ya nchi ya Tanzania na mazao ambayo huzalishwa katika mikoa hiyo. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa wastani kwa sababu ni watahiniwa 381,786 (41.63%) walichagua jibu sahihi ambalo ni *A*, *Kagera, Kilimanjaro na Mbeya*. Uchaguzi wa jibu hili sahihi unamaanisha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa hali ya hewa inayohitajika katika kilimo cha ndizi ambayo ni ya baridi na mvua au unyevu wa wastani ambayo inapatikana katika mikoa ya Kagera, Kilimanjaro na Mbeya.

Jumla ya watahiniwa 158,198 (17.25) walichagua B, *Mbeya Kagera na Lindi.* Hata hivyo, kati ya mikoa hiyo zao la ndizi halilimwi katika mkoa wa Lindi kutokana na hali ya hewa ya kipindi kimoja cha mvua. Watahiniwa 154,382 (16.83%) walichagua *D*, *Arusha, Morogoro na Shinyanga*. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa pamoja na ukweli kwamba ndizi zinalimwa pia katika mikoa ya Arusha na Morogoro, zao hilo halilimwi katika mkoa wa Shinyanga kwa sababu una hali ya hewa ya nusu jangwa. Watahiniwa wengine 208,257 (22.82%) walichagua vipotoshi *C*, *Kagera, Singida na Shinyanga* na *E*, *Singida, Lindi na Kagera* kwa kuwa vilihusisha

Mkoa wa Kagera ambao unalima ndizi. Watahiniwa hao hawakubaini kuwa hali ya hewa ya mikoa ya Singida, Lindi na Shinyanga hairuhusu kilimo cha ndizi. Watahiniwa 13,461 (1.5%) hawakujibu swali hili na wengine walichagua zaidi ya jibu moja kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 17.




**Kielelezo Na. 2.17:** *kinaonesha magawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo ambapo kiwango cha kufaulu ni cha wastani.*

**Swali la 41:** Kiasi cha mvua wastani wa milimeta 500 kwa mwaka, joto kali mchana kati ya nyuzi joto 28 hadi 30 na baridi kali usiku ni sifa za hali ya hewa ya

| | | | |
|---|---|---|---|
| A | Kitropiki | B | Jangwa |
| C | Nusu Jangwa | D | Kiikweta |
| E | Kimediteraniani. | | |

Swali lilipima uelewa wa mtahiniwa katika kutofautisha sifa za tabia nchi za maeneo mbalimbali. Watahiniwa walitakiwa kubainisha tabia

ya nchi yenye kiasi cha mvua cha wastani wa milimita 500 kwa mwaka, joto kali mchana kati ya nyuzi joto 28 hadi 30 na baridi kali sana usiku. Kwa jumla kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa hafifu kwani ni watahiniwa 163,068 (17.78%) walichagua jibu sahihi *B*, *Jangwa*. Watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu sifa mbalimbali za tabia nchi ya Jangwa. Watahiniwa 193,668 (21.12%) walichagua kipotoshi *A*, *kitropiki.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa tabia nchi ya kitropiki imetawaliwa na joto la wastani mchana na usiku. Jumla ya watahiniwa 184,448 (20.11%) walichagua kipotoshi *C, nusu jangwa*. Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha sifa za jangwa na nusu jangwa kwani sifa nyingi zinafanana. Tofauti ipo katika kiwango cha mvua ambapo nusu jangwa hupata mvua kuliko katika tabia nchi ya jangwa ambapo mvua ni kidogo zaidi kuliko ilivyo katika hali ya nusu jangwa ambapo hupata mvua kufikia milimita 750 japo si za kuaminika. Kwa upande mwingine, watahiniwa 222,008 (24.21%) waliochagua kipotoshi *D*, *kiikweta* walishindwa kubaini kuwa tabia nchi ya kiikweta imetawaliwa na mvua nyingi na joto kali mwaka mzima. Vilevile, watahiniwa 138,605 (15.11%) waliochagua kipotoshi *E*, *kimediteraniani* walishindwa kuelewa kuwa tabia nchi ya kimediteraniani hupata mvua msimu wa baridi wakati sehemu nyingine mvua zinanyesha msimu wa joto. Watahiniwa 15,269 (1.70%) wahakujibu swali hili.

Chunguza kwa umakini picha ifuatayo kisha jibu swali la 42 na 43.




**Swali la 42:** Shughuli kuu ya kiuchumi inayoweza kufanyika katika eneo hili ni

A kilimo
B ufugaji
C uvuvi
D utalii
E viwanda.

Katika swali hili, watahiniwa walipaswa kuchunguza na kutafsiri picha iliyooneshwa ili kubaini shughuli kuu ya kiuchumi inayoweza kufanyika katika eneo husika. Watahiniwa wengi walikuwa na uelelewa wa swali hili kwani zaidi ya nusu ya watahiniwa 668,057 (72.85%) waliweza kuchagua jibu sahihi *D*, *Utalii*. Kufaulu huku kunadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na ufahamu wa kusoma picha na kuitafsiri kwa ufasaha. Hata hivyo, watahiniwa 143,246 (15.62%) walichagua kipotoshi *B, ufugaji.* Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha wanyama wa porini na wa kufugwa kwani wanyama wanaoonekana katika picha ni wanyama pori kuashiria kuwa sehemu iliyopigwa picha ni mbuga ambako sehemu za ufugaji haziruhusiwi.

Kwa upande mwingine watahiniwa 74,625 (8.14%) walichagua vipotoshi *A*, *Kilimo* na *C, Uvuvi.* Watahiniwa hao walikosa ufahamu wa viashiria vya ufanyikaji wa shughuli hizi za kiuchumi katika eneo lililoonyeshwa katika picha kwani hakukuwa na viashiria vyovyote vya utendekaji wa shughuli hizo katika picha. Watahiniwa 19,986 (2.18%) walishindwa kuelewa matakwa ya swali kwani walichagua kipotoshi *E*, *viwanda* wakati picha ilionesha wanyama pori. Aidha, watahiniwa 11,170 (1.22%) hawakujibu swali hili kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 2.18 hapa chini.




**Kielelezo Na. 2.18:** *Asilimia ya watahiniwa walivyochagua kila chaguo katika swali la 42.*

**Swali la 43:** Moja ya manufaa ya wanyama wanaoonekana katika picha ni

A kuongezeka kwa idadi ya wanyama pori
B uhifadhi wa mazingira
C kuongezeka kwa pato la nchi
D ongezeko la misitu
E ongezeko la mvua.

Swali hili pia lilihusiana na swali la 42 lililoonyesha picha ya mbuga ya wanyama ambapo watahiniwa walitakiwa kuitafsiri na kutambua shughuli ya kiuchumi inayoweza kuendeshwa katika mazingira hayo. Katika swali la 43, watahiniwa walipimwa maarifa yao kuhusu manufaa ya wanyama wanaoonekana katika picha. Hili ni moja kati ya maswali ambayo yalikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa sababu zaidi ya nusu ya watahiniwa 573,191 (62.50%) waliojibu swali hili, waliweza kuchagua jibu sahihi *C*, *kuongezeka kwa pato la nchi*. Watahiniwa hao walionyesha ujuzi mkubwa waliokuwa nao kuhusu utalii na faida ya shughuli za utalii nchini. Hata hivyo, watahiniwa 169,187 (18.45%) waliochagua kipotoshi *A, kuongezeka kwa idadi ya wanyama pori* walishindwa kuelewa kuwa swali liliwataka kubainisha manufaa ya wanyama pori. Vile vile watahiniwa 81,704 (8.91%) waliochagua kipotoshi *B, uhifadhi wa mazingira* walishindwa kufahamu kuwa wanyama pori hawana uwezo wa kuhifadhi mazingira. Pia, shughuli za utalii katika mbuga za wanyama zisipodhibitiwa, husababisha uchafuzi wa mazingira.

Watahiniwa 46,914 (5.12%) waliochagua kipotoshi *D, ongezeko la misitu* walishindwa kuelewa kuwa baadhi ya wanyama pori wanakula matawi ya miti na majani, hivyo kusababisha upotevu wa misitu au kuhatarisha ustawi wa mimea. Jumla ya watahiniwa 34,241 (3.73%) waliochagua kipotoshi *E, ongezeko la mvua* walionyesha kuwa hawakuelewa matakwa ya swali kwani hakuna uhusiano wowote wa uwepo wa wanyama pori na ongezeko la mvua. Aidha, watahiniwa 11,847 (1.30%) hawakufanya swali hili.

**Swali la 44:** Lipi kati ya majanga yafuatayo linasabishwa na binadamu?

A Vita
B Ukame
C Mlipuko wa Volkano
D Tetemeko la ardhi
E Kimbunga.

Lengo la swali lilikuwa kupima ufahamu wa mtahiniwa kuhusu majanga yanayoweza kusababishwa na binadamu. Watahiniwa wengi 628,506 (68.53%) walichagua *A, Vita* ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa hao waliweza kubaini jibu sahihi huenda kwa sababu janga la Vita linajitokeza sana katika jamii na kutangazwa na vyombo mbalimbali vya habari. Pia, madhara ya vita ambayo ni vifo na ukimbizi yaliwafanya watahiniwa kuyakumbuka kwa urahisi.

Jumla ya watahiniwa 166,413 (18.15%) waliovutiwa na kipotoshi *B*, *Ukame* walishindwa kubaini kuwa ukame ni janga ambalo linaweza kusababishwa na nguvu za asili au shughuli za kibinadamu kama kilimo cha kuhamahama na ufugaji wa kuhamahama. Kwa upande mwingine, watahiniwa 41,947 (4.57%) waliochagua kipotoshi *C, mlipuko wa volcano*; watahiniwa 42,394 (4.62%) waliochagua *D, tetemeko la ardhi* na watahiniwa 26,326 (2.87%) waliochagua *E*, *kimbunga* walishindwa kutofautisha majanga ambayo ni ya asili na yale yanayosababishwa na wanadamu. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ni ishara kuwa mada ya majanga haikueleweka kwa kiwango kikubwa. Watahiniwa 11,498 (1.25%) waliobaki hawakujibu swali hili.

**Swali la 45:** Katani, chai na kahawa ni

A mazao ya chakula
B mazao ya biashara
C mazao ya mikundekunde
D mazao ya muda mfupi
E mazao ya kusafirisha nje.


Swali hili lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa juu ya makundi ya mazao. Ili mtahiniwa aweze kujibu vema swali hili alitakiwa kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu makundi mbalimbali ya mazao na matumizi yake. Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha kundi linalojumuisha mazao ya Katani, Chai na Kahawa. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kuzuri kwani zaidi ya robo tatu ya watahiniwa 764,249, (83.33%) walichagua jibu sahihi *B*, *mazao ya biashara* kwa sababu walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu aina za mazao na matumizi yake.

Hata hivyo, watahiniwa 44,540 (4.86%) waliochagua *A*, *mazao ya chakula* walivutiwa na chai na kahawa ambayo ni mazao ya chakula wakasahau kuwa katani haitumiwi kama chakula. Watahiniwa wengine 36,159 (3.94%) walichagua *C*, *mazao ya mikundekunde*. Watahiniwa hao walishindwa kuchagua jibu sahihi kutokana na kuwa na uelewa mdogo wa aina za mazao na matumizi yake au hawakujua maana ya mazao ya mikundekunde.

Watahiniwa wengine 30,139 (3.29%) walichagua *D*, *mazao ya muda mfupi*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki unaonesha wazi kuwa watahiniwa hao walikuwa hawana uelewa kuwa mazao ya katani, chai na kahawa ni mazao ambayo huchukua muda kuanzia kupandwa mpaka kuvunwa.

Aidha, watahiniwa 30,947 (3.37%) waliochagua *E*, *mazao ya kusafirisha nje* walishindwa kubaini kuwa mazao ya biashara na yale ya chakula yote yanaweza kusafirishwa nje ya nchi. Pia, hawakuwa na uelewa kuwa mazao ya katani, chai na kahawa hutumika pia katika viwanda vya ndani ya nchi. Watahiniwa wengine 11,050

(1.20%), hawakujibu swali hili kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 2.19 hapa chini.




**Kielelezo Na. 2.19:** *Asilimia ya watahiniwa walivyochagua katika kila chaguo katika swali la 45.*

**Swali la 46:** Ranchi ni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya

A kilimo cha mazao
B kuchinjia wanyama
C kufugia wanyama
D kuogeshea wanyama
E kuotesha nyasi.

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha matumizi sahihi ya maeneo ya ranchi. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa wastani kwani watahiniwa 464,052 (50.60%) walichagua *C*, *kufugia wanyama* ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa walioweza kubaini jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya neno ranchi ambayo ni njia ya ufugaji wa kisasa ambapo wanyama wanafugwa kwa uhuru katika shamba kubwa katika ardhi

iliyo wazi. Kwa upande mwingine, watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa ranchi mbalimbali zinazopatikana nchini Tanzania, kama vile Ruvu mkoani Pwani, Azimio mkoani Tanga, Dakawa mkoani Morogoro na Kongwa mkoani Dodoma.

Jumla ya watahiniwa 101,911 (11.11%) walichagua kipotoshi A, *kilimo cha mazao*. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa Ranchi inahusika na ufugaji wa wanyama na si vinginevyo. Watahiniwa wengine 100,424 (11.0%) waliochagua *B*, *kuchinjia wanyama* walionekana kutokuwa na maarifa kuhusu utofauti kati ya maeneo ya ranchi na machinjio ya wanyama. Mara nyingi, maeneo ya machinjio ya wanyama yametengwa maalum kwa ajili ya kuchinja tu na sio kufugia wanyama.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiuniwa 125,404 (13.67%) walichagua *D*, *kuogeshea wanyama*. Watahiniwa hao hawakuweza kubaini makusudi makubwa ya ranchi kuwa sio kuwapeleka wanyama wakaoge ila ni kwa kufugia wanyama. Vilevile watahiniwa 111,554 (12.16%) walichagua *E*, *kuotesha nyasi* ambalo siyo kusudio kubwa la kutenga maeneo ya ranchi. Watahiniwa 13,739 (1.50%) hawakujibu swali hili.

**Swali la 47:** Katika Afrika kondoo wa sufu wanafugwa kwa wingi katika nchi ya

A Namibia
B Tanzania
C Afrika ya Kusini
D Lesotho
E Botswana.

Swali hili lilipima uwezo wa mtahiniwa kubaini nchi inayofuga kondoo wa sufu kwa wingi katika Afrika. Kufaulu kwa watahiniwa

katika swali hili kulikuwa kwa wastani kwa sababu watahiniwa 496,038 (54.09%) waliweza kuchagua *C*, *Afrika ya Kusini* ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa hao waliweza kuchagua jibu sahihi kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya ufugaji wa kondoo wa sufu katika Afrika.

Watahiniwa wengine 100,370 (10.94%) walivutiwa na kipotoshi *A*, *Namibia* kutokana na kukosa uelewa mzuri juu ya ufugaji wa kondoo wa sufu katika Bara la Afrika. Vilevile, watahinwa 76,932 (8.39%) walichagua kipotoshi *B*, *Tanzania*. Watahiniwa hao wanaweza kuwa walichagua Tanzania kutokana na ukweli kuwa kondoo wa sufu wanafugwa pia hapa nchini katika wilaya ya Makete. Hata hivyo, walishindwa kubaini kuwa hapa nchini kondoo hao wanafugwa kwa kiwango kidogo sana.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 91,269 (9.95%) waliochagua *D*, *Lesotho* na watahiniwa 138,976 (15.15%) waliochagua *E*, *Botswana* walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ufugaji wa kondoo wa sufu katika Bara la Afrika. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaweza kuwa ulisababishwa na ukweli kuwa nchi za Lesotho na Botswana zinapatikana kusini mwa Bara la Afrika na zinapakana na nchi ya Afrika ya Kusini. Watahiniwa wengine 13,499 (1.47%) hawakujibu swali hili.

**Swali la 48:** Uvuvi **usio** endelevu hufanyika kwa kutumia

| | | |
|---|---|---|
| A mitego | B meli kubwa | C kokoro |
| D ndoano | E nyavu kubwa. | |

Katika kulijibu swali hili mtahiniwa alitakiwa kubaini njia zinazotumiwa kufanya uvuvi usio endelevu. Kufaulu kwa watahiniwa

katika swali hili kulikuwa kwa wastani kwani ni watahiniwa 380,749 (41.52%) walichagua jibu sahihi *C*, *kokoro*. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu njia mbalimbali za uvuvi usio endelevu. Kipotoshi *A*, *mitego* kilivutia 20.36% ya watahiniwa. Pengine hii inatokana na matumizi ya aina mbalimbali za mitego kama vile vikapu na ndoano katika uvuvi wa kawaida wa wavuvi wadogo wadogo katika mazingira yao ya kila siku.

Kundi jingine la watahiniwa 75,575 (8.24%) walivutiwa na kipotoshi B, *Meli kubwa* bila kufahamu kuwa Meli kubwa zinatumika kuvua samaki wakubwa katika bahari kuu. Hii ni njia sahihi ya uvuvi inayokubaliwa tofauti na ile ya wavuvi wadogowadogo wanaotumia kokoro kuhatarisha mazalia ya samaki.

Watahiniwa wengine 193,165 (21.06%) walichagua vipotoshi *D*, *ndoano* na 68,104 (7.43%) walichagua *E*, *nyavu kubwa*. Watahiniwa kuchagua vipotoshi hivi kunaonesha kuwa hawakuwa makini kulisoma swali kwani hizi pia ni njia za uvuvi salama zinazoshauriwa kutumika. Pengine hawa hawakuwa na uelewa sahihi kuhusu dhana ya uvuvi usio endelevu. Aidha, watahiniwa 12,809 (1.40%) hawakujibu swali hili.

**Swali la 49:** Ni madini gani yanapatikana nchini Tanzania pekee?

A Dhahabu. B Urani. C Almasi.
D Tanzanaiti E Shaba.

Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kuchagua madini yanayopatikana nchini Tanzania pekee. Swali hili ni kati ya maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi kwani watahiniwa 641,530

(69.95%) walichagua *D*, *Tanzanaiti* ambalo ndilo jibu sahihi. Kwa kuchagua Tanzanaiti, inaonesha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu mzuri kuhusu aina mbalimbali za madini na mtawanyiko wa upatikanaji wake duniani licha ya ukweli kuwa Tanzanaiti ina mfanano na jina la nchi ya Tanzania.


Watahiniwa wengine 91,975 (10.03%) waliochagua kipotoshi *A*, *dhahabu* walishindwa kuelewa kuwa swali liliwataka kuchagua madini yanayopatikana Tanzania pekee, pamoja na ukweli kuwa dhahabu hupatikana pia nchini Tanzania. Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua *B*, *urani* (4.38%), *C Almasi* (9.71%) na *E*, *Shaba* (4.69%) waliamua kuchagua jibu lolote bila kufuata matakwa ya swali. Hata hivyo, 1.24% ya watahiniwa hawakujibu swali hili.

**Swali la 50:** Usafirishaji wa bidhaa au watu kupeleka mahali pengine huitwa

A uchukuzi B utalii
C biashara D mawasiliano
E uhamaji.

Katika kujibu swali hili, watahiniwa walitakiwa kuwa na maarifa ya mada ya mawasiliano, biashara na uchukuzi. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kuzuri kwani watahiniwa wengi 553,853 (60.39%) walichagua *A, uchukuzi* ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhushu shughuli mbalimbali zinazofanywa katika kufanikisha maendeleo. Pia, walikuwa na ufahamu wa shughuli za uchukuzi kwa kuwa katika maisha yao ya kila siku wanatumia vyombo mbalimbali vya uchukuzi kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine vyombo hivyo ni kama vile baisikeli, pikipiki na magari.

Watahiniwa wengine 60,369 (6.58%) waliochagua *B*, *utalii* walikuwa na uelewa wa jumla kuhusu utalii. Hata hivyo, walishindwa kuelewa kuwa uchukuzi ndio huwezesha shughuli za utalii kufanyika kwa ufasaha. Jumla ya watahiniwa 292,347 (31.88%) walichagua vipotoshi *C*, *biashara*, *D*, *mawasiliano* na *E, uhamaji*. Watahiniwa hao walichagua vipotoshi hivyo kutokana na kushindwa kutofautisha dhana ya uchukuzi na biashara, mawasiliano na uhamiaji. Watahiniwa hao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu usafirishaji wa bidhaa au watu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Watahiniwa wengine 10,515 (1.15%) hawakujibu swali hili kama inavyooneshwa katika Kielelez0 2.20 hapa chini.




**Kielelezo Na. 2.20:** *Asilimia ya watahiniwa walivyochagua katika kila chaguo katika swali la 50 ambapo kufaulu kwa watahiniwa ni kwa kiwango cha wastani.*

## 3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA

Mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii ulikuwa na jumla ya mada **30**. Uchambuzi wa kiwango cha kufaulu katika somo hili unaonesha kuwa kwa jumla, Ikilinganishwa na mwaka 2016, kiwango cha kufaulu katika mwaka 2017 kimeshuka. Hata hivyo, mada **07** zilikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu, mada **13** zilikuwa na kiwango cha wastani na mada **10** zilikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu.

Ulinganifu wa kiwango cha kufaulu kati ya mwaka 2017 na 2016 unaonesha kuwa, baadhi ya mada zimekuwa na ongezeko la kiwango cha kufaulu. Katika mada ya *Utamaduni Wetu* kiwango cha kufaulu kimeongezeka kwa asilimia **25.77** kutoka wastani kuwa kizuri na mada ya *Usomaji wa Ramani* kiwango cha kufaulu kimeongezeka kutoka hafifu kwenda wastani. Mada ya *Majanga* na *Maji* imebadilika kutoka kiwango hafifu kuwa kizuri kwa asilimia **41.78** na **45.96** mtawalia.

Kwa upande mwingine, kiwango cha kufaulu katika mada **03** kimeshuka kutoka kizuri kwenda hafifu. Mada hizo ni *Uchumi Wetu kwa* asilimia **57.42**, *Familia Yetu* asilimia **37.42** na *Harakati za Kupigania Uhuru katika Afrika* asilimia **49.77.** Aidha, kiwango cha kufaulu katika mada ya *Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Zingine za Kiasia na Kizungu* ulishuka kutoka wastani kwenda hafifu. Kimsingi, mada ambazo ufaulu wake umebakia kuwa mzuri ni **04** nazo ni; *Demokrasia, Vitangulizi vya Ukoloni, Tafsiri za Picha na Ramani, Mawasiliano na Biashara na Uchukuzi*. Mada ambazo

kufaulu kwake kumebakia kuwa hafifu ni **02** nazo ni *Ushirikiano kati ya Tanzania na Mataifa Mengine* na *Biashara ya Utumwa*.

Ili kuinua na kuboresha kufaulu katika somo hili ni vema msisitizo uongezwe katika ufundishaji wa mada zote. Aidha, mada ya *Ushirikiano kati ya Tanzania na Mataifa Mengine* na *Biashara ya Utumwa* ambazo kiwango chake cha kufaulu kimekuwa hafifu kwa miaka miwili mfululizo, zitiliwe mkazo zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wake.

**Jedwali Na 4: Mada Zilizoonesha Ongezeko la Kufaulu kwa Watahiniwa**

| Na. | Mada | Wastani wa Waliofaulu 2016 (%) | Wastani wa Waliofaulu 2017 | Wastani wa Ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Utamaduni wetu | 43.83 | 69.6 | 25.77 |
| 2. | Vitangulizi vya ukoloni | 61.02 | 74.1 | 13.08 |
| 3. | Ushirikiano wa Kimataifa | 53.20 | 58.9 | 5.7 |
| 4. | Majanga | 26.72 | 68.5 | 41.78 |
| 5. | Maji | 19.54 | 65.5 | 45.96 |
| 6. | Usomaji wa ramani | 21.95 | 42.8 | 20.85 |

**Jedwali Na. 5: Mada Zilizoonesha Kushuka kwa Kufaulu kwa Watahiniwa**

| Na. | Mada | Wastani wa Waliofaulu 2016 (%) | Wastani wa Waliofaulu 2017 (%) | Wastani wa Ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Serikali za Mitaa | 49.36 | 34.5 | 14.86 |
| 2. | Serikali Kuu | 78.28 | 47.9 | 30.38 |
| 3. | Demokrasia | 68.60 | 60.5 | 8.1 |

| Na. | Mada | Wastani wa Waliofaulu 2016 (%) | Wastani wa Waliofaulu 2017 (%) | Wastani wa Ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|
| 4. | Alama za Taifa | 72.32 | 50.0 | 22.32 |
| 5. | Ulinzi na Usalama katika Shule | 49.41 | 47.5 | 1.91 |
| 6. | Uchumi Wetu | 72.52 | 15.1 | 57.42 |
| 7. | Ushirikiano Kati ya Tanzania na Mataifa Mengine | 29.08 | 20.5 | 8.58 |
| 8. | Katiba ya Jamhuri ya Tanzania | 58.79 | 43.5 | 15.29 |
| 9. | Familia Yetu | 70.42 | 33 | 37.42 |
| 10. | Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu | 58.77 | 31.9 | 26.87 |
| 11. | Biashara ya Watumwa | 39.89 | 28.2 | 11.69 |
| 12. | Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar | 54.68 | 44.8 | 9.88 |
| 13. | Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika Kuanzia mwaka 1880 | 54.69 | 33.45 | 21.24 |
| 14. | Harakati za Kupigania Uhuru katika Afrika | 71.67 | 21.9 | 44.77 |
| 15. | Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru | 48.02 | 44.32 | 3.7 |
| 16. | Tafsiri ya ramani na picha | 75.77 | 67.6 | 8.17 |
| 17. | Mawasiliano, Biashara na | 74.25 | 71.85 | 2.4 |

| Na. | Mada | Wastani wa Waliofaulu 2016 (%) | Wastani wa Waliofaulu 2017 (%) | Wastani wa Ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|
| | Uchukuzi | | | |
| 18. | Mazingira | 69.91 | 52.45 | 17.46 |
| 19. | Shughuli za kiuchumi | 67.48 | 51.56 | 5.92 |

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya watahinwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii umeonesha kushuka kwa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa jumla. Kufaulu kwa watahiniwa katika mada 25 zilizotahiniwa mwaka 2016 na 2017 kumeonesha kushuka isipokuwa katika mada sita ambazo ni *Utamaduni Wetu, Vitangulizi vya Ukoloni, Ushirikiano wa Kimataifa, Majanga, Maji* na *Usomaji wa Ramani*.

Kushuka kwa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kumeonekana katika mada kumi na tisa. Miongoni mwa mada hizo, zipo ambazo kiwango cha kufaulu kilishuka kutoka kiwango kizuri kwenda kiwango cha wastani (*Serikali Kuu, Alama za Taifa, Mazingira na Shughuli za Kiuchumi*), kiwango kizuri kwenda kiwango hafifu (*Familia Yetu, Uchumi Wetu* na *Harakati za Kupigania Uhuru katika Afrika*) na zingine zilishuka kutoka kufaulu kwa kiwango cha wastani kwenda kiwango hafifu (*Serikali za Mitaa, Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika Kuanzia mwaka 1880* na *Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu*). Aidha, mada za *Ushirikiano Kati ya Tanzania na Mataifa Mengine* na *Biashara ya Watumwa*

zilikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu mwaka 2016 na zimeendelea kubaki katika kiwango hicho.

Kwa upande mwingine, mada za *Majanga* na *Maji* kufaulu kwa watahiniwa kuliongezeka kutoka kiwango hafifu kuwa kiwango kizuri.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha elimu, hususan kufaulu kwa watahiniwa, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Walimu wanaofundisha masomo ya Uraia, Historia na Jiografia yanayounda mtihani wa Maarifa ya Jamii katika shule za Msingi wanatakiwa kufundisha mada zote kwa ukamilifu kama zinavyooneshwa kwenye muhtasari.

(b) Walimu na wanafunzi wabaini mada zilizokuwa na ufaulu wa chini katika mtihani wa mwaka huu na kuziongezea bidii ili ziweze kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu katika mitihani ya miaka ijayo.

(c) Wanafunzi washauriwe na kusisitiziwa kusoma kwa uelewa vitabu vya kiada na ziada ili kuongeza maarifa na ujuzi ambao utawawezesha kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi.

(d) Mamlaka husika ziendelee kufanya ufuatiliaji katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo Uraia, Historia na Jiografia, hasa katika mada kumi na tisa (19) ambazo kufaulu kwa watahiniwa kumeshuka ili kubaini changamoto zinazozuia ufanisi katika ujifunzaji na ufundishaji na kuziondoa ili kuongeza kiwango cha kufaulu.

## Ulinganifu wa Kufaulu kwa Watahiniwa katika kila Mada kwa Mwaka 2016 na 2017

| Na | Mada | Mtihani wa 2016 | | | | Mtihani wa 2017 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| | | Namba ya swali | Asilimia ya Ufaulu | | | Namba ya swali | Asilimia ya Ufaulu | | |
| 1. | Serikali za Mitaa | 1<br>2 | 75.61<br>23.11 | 49.36 | Wastani | 1<br>3 | 47.9<br>21.1 | 34.5 | Hafufu |
| 2. | Serikali Kuu | 3 | 78.28 | 78.28 | Vizuri | 2 | 47.9 | 47.9 | Wastani |
| 3. | Demokrasi a | 6<br>7<br>8 | 80.26<br>44.16<br>12.77 | 68.60 | Vizuri | 9<br>10 | 56.6<br>64.3 | 60.5 | Vizuri |
| 4. | Alama za Taifa | 4<br>5 | 69.52<br>75.11 | 72.32 | Vizuri | 4<br>5 | 85.2<br>14.9 | 50.0 | Wastani |
| 5. | Ulinzi na Usalama katika Shule/Taifa | 9<br>10 | 37.74<br>61.08 | 49.41 | Wastani | 6<br>7 | 24.2<br>70.8 | 47.5 | Wastani |
| 6. | Uchumi Wetu | 11 | 72.52 | 72.52 | Vizuri | 12 | 15.1 | 15.1 | Hafufu |
| 7. | *Utamaduni Wetu | 12 | 43.83 | 43.83 | Wastani | 11 | 69.6 | 69.6 | Vizuri |
| 8. | Ushirikiano kati ya Tanzania na Mataifa mengine | 14 | 29.08 | 29.08 | Hafifu | 14 | 20.5 | 20.5 | Hafifu |
| 9. | Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | 13 | 58.79 | 58.79 | Wastani | 13 | 43.5 | 43.5 | Wastani |
| 10. | *Familia Yetu | 15<br>17 | 57.01<br>83.84 | 70.42 | Mzuri | - | - | - | - |
| 11. | *ShuleYetu | 16 | 83.32 | 83.32 | Mzuri | - | - | - | - |
| 12. | Misingi ya demokrasia | - | - | - | - | 8 | 54.8 | 54.8 | Wastani |
| 13. | FamiliaYetu | 15<br>17 | 57.01<br>83.84 | 70.42 | Vizuri | 15 | 33 | 33 | Hafifu |
| 14. | *ShuleYetu | 16 | 83.32 | 83.32 | Vizuri | - | - | - | - |
| 15. | *Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu | 20 | 56.96 | 56.96 | Wastani | - | - | - | - |
| 16. | *Mahusiano Miongoni | 21 | 54.21 | 54.21 | Wastani | - | - | - | - |

| Na | Mada | Mtihani wa 2016 | | | | Mtihani wa 2017 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| | | Namba ya swali | Asilimia ya Ufaulu | | | Namba ya swali | Asilimia ya Ufaulu | | |
| | mwa Jamii za Tanzania hadi Karne ya 19 | | | | | | | | |
| 17. | Hatua za Maendeleo ya Binadamu Katika Zama Mbalimbali | 18<br>19 | 73.64<br>26.03 | 49.83 | Wastani | - | - | - | - |
| 18. | Kukua kwa Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala Katika Jamii za Kitanzania hadi Karne ya 19. | - | - | - | - | 16<br>17 | 31.5<br>52.2 | 43.35 | Wastani |
| 19. | Utamaduni | - | - | - | - | 19<br>20 | 35.3<br>37.2 | 36.25 | Hafifu |
| 20. | Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Afrika | 23 | 38.13 | 38.13 | Hafifu | - | - | - | - |
| 21. | Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu | 22 | 58.77 | 58.77 | Wastani | 22 | 31.9 | 31.9 | Hafifu |
| 22. | Biashara ya Watumwa | 24 | 39.89 | 39.89 | Hafifu | 18<br>23 | 23.8<br>32.6 | 28.2 | Hafifu |
| 23. | Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Tanganyika na Zanzibar | 25 | 68.95 | 68.95 | Vizuri | - | - | - | - |

| Na | Mada | Mtihani wa 2016 | | | | Mtihani wa 2017 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| | | Namba ya swali | Asilimia ya Ufaulu | | | Namba ya swali | Asilimia ya Ufaulu | | |
| 24. | Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar | 27 | 54.68 | 54.68 | Wastani | 31 | 44.8 | 44.8 | Wastani |
| 25. | Vitangulizi vya Ukoloni | 26 | 61.02 | 61.02 | Vizuri | 24 | 74.1 | 74.1 | Vizuri |
| 26. | Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika Kuanzia Mwaka 1880 | 31 | 54.69 | 54.69 | Wastani | 25 | 47.5 | 33.45 | Wastani |
| | | | | | | 27 | 19.4 | | |
| 27. | Harakati za Kupigania Uhuru katika Afrika | 29 | 71.67 | 71.67 | Vizuri | 26 | 21.9 | 21.9 | Hafifu |
| 28. | Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru | 28 | 48.02 | 48.02 | Wastani | 28 | 59.3 | 44.32 | Wastani |
| | | | | | | 29 | 49.9 | | |
| | | | | | | 30 | 42.6 | | |
| | | | | | | 32 | 25.5 | | |
| 29. | Ushirikiano wa Kimataifa | 30 | 49.26 | 53.20 | Wastani | 21 | 58.9 | 58.9 | Wastani |
| | | 32 | 57.15 | | | | | | |
| 30. | Tafsiri za Picha na Ramani. | 40 | 93.64 | 75.77 | Vizuri | 42 | 72.8 | 67.6 | Vizuri |
| | | 41 | 83.93 | | | 43 | 62.5 | | |
| | | 42 | 49.74 | | | | | | |
| 31. | Mawasiliano, biashara na uchukuzi | 43 | 75.54 | 74.25 | Vizuri | 45 | 83.3 | 71.85 | Vizuri |
| | | 44 | 83.87 | | | 50 | 60.4 | | |
| | | 45 | 75.49 | | | | | | |
| | | 46 | 80.97 | | | | | | |
| | | 47 | 55.4 | | | | | | |
| 32. | Mazingira | 33 | 87.18 | 69.91 | Vizuri | 33 | 84.7 | 52.45 | Wastani |
| | | 36 | 74.23 | | | | | | |

| Na | Mada | Mtihani wa 2016 | | | | Mtihani wa 2017 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| | | Namba ya swali | Asilimia ya Ufaulu | | | Namba ya swali | Asilimia ya Ufaulu | | |
| | | 49 | 72.8 | | | 37 | 20.2 | | |
| | | 48 | 33.42 | | | | | | |
| 33. | Shughuli za Kiuchumi | 34 | 83.9 | 67.48 | Vizuri | 40 | 41.6 | 51.56 | Wastani |
| | | 38 | 69.72 | | | 46 | 50.6 | | |
| | | 39 | 48.83 | | | 47 | 54.1 | | |
| | | | | | | 48 | 41.5 | | |
| | | | | | | 49 | 70.0 | | |
| 34. | Majanga | 37 | 26.72 | 26.72 | Hafifu | 44 | 68.5 | 68.5 | Vizuri |
| 35. | Usomaji wa ramani | 35 | 21.95 | 21.95 | Hafifu | 34 | 51.1 | 42.8 | Wastani |
| | | | | | | 38 | 50.3 | | |
| | | | | | | 39 | 27.1 | | |
| 36. | Maji | 50 | 19.54 | 19.54 | Hafifu | 36 | 65.5 | 65.5 | Vizuri |
| 37. | Mfumo wa Jua | - | - | - | - | 35 | 20.0 | 20.0 | Hafifu |
| 38. | Hali ya hewa | - | - | - | - | 41 | 17.8 | 17.8 | Hafifu |